BREAKING NEWS
SUPA JACKPOT
1,004,055,092/-
KWA 1000/- TU!
SportPesa.CO.TZ PIGA *150*87#



UKURASA 19

**MBARONI** tuhuma kuua mumewe kwa kumkaba




MLEZI PEKEE BIBI YAO KIKONGWE...

**Yatima wenye njaa, nyumba nusura kubomoka, hadi Diwani kuwaopoa**

Ijumaa Juni 10, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580972

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper


LIKE & FOLLOW US

UKURASA 11

# MSHTUKO

**WAZIRI** wa Elimu abaini 'madudu' shuleni...*Endelea Ukurasa 2*

**WANAFUNZI** 600 matundu mawili ya choo



**KITANDA** kimoja kwa wanafunzi wawili



**DARASANI** mwalimu mmoja wanafunzi 104



**USHUHUDA** wa maadili waichefua wizara




**ASHIKIA** bango wahitimu wake kutoajirika




**UKAGUZI** duni shuleni, shida inayojitegemea





Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda

## Bunge laipa serikali miezi 3 majibu mauaji hifadhini

UKURASA 3



## Rais Samia aagiza benki zishushe riba za mikopo

UKURASA 2

Rais Samia Suluhu Hassan, akifungua pazia kuzindua awamu ya tatu ya upanuzi wa mashamba ya Kampuni ya Kagera Sugar, Kitengule wilayani Karagwe mkoani Kagera jana. Wengine ni Mwenyekiti wa Bodi ya Kagera Sugar, Seif Ali Seif (wapili kushoto), Mkurugenzi wa Bodi ya Kagera Sugar, Nassoro Ali (kushoto), Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe (kushoto kwa Rais) na Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Dk. Ashatu Kijaji. **PICHA: SELEMAN MPOCHI**

**MICHEZO** **BINGWA LIGI KUU BARA KUSOMBA SH. MIL. 600** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6




Mkurugenzi wa Taasisi ya Aisha Sururu Foundation (ASF), Aisha Sururu (kushoto), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam juzi, kuhusu kuunga mkono juhudi za Rais Samia Suluhu Hassan, kupinga ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto. Kulia ni Mbunge wa Viti Maalum CCM, Zainab Vullu. **PICHA: JUMANNEJUMA**

# Mshtuko ufuatiliaji ubora wa elimu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

NI mshtuko! Ndivyo unavyoweza kutafsiri kutokana na kile alichokibaini Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, kwenye ufuatiliaji wa uendeshaji wa shule na ubora wa elimu nchini.

Msimamizi huyo wa elimu nchini mbali na mambo mengine, amebaini zipo shule ambazo kiuhalisia hazikupaswa kupewa kibali cha kutoa huduma ya elimu kutokana na kutokidhi matakwa ya kisheria na miongozo iliyowekwa, lakini zinaendelea kutoa huduma hiyo katika mazingira ambayo ni dhahiri ubora wa elimu inayotolewa una ukakasi.

Miongoni mwa dosari alizobaini ni shule yenye wanafunzi 600 lakini wanatumia matundu mawili ya vyoo.

Kwa mujibu wa miongozo iliyopo nchini, tundu moja la choo linapaswa kutumiwa na wanafunzi 25 wa kiume na 20 wa kike, hivyo shule hiyo yenye wanafunzi 600 kama ni wavulana ilipaswa kuwa na matundu 24 na kama ni wasichana ilipaswa kuwa na matundu 30.

Waziri Mkenda alibainisha hayo juzi kwenye kikao kazi cha tathmini ya utendaji kazi idara ya udhibiti ubora wa shule kwa viongozi wa kanda na wilaya nchini kilichofanyika jijini hapa.

"Kuna siku nilisema tunakwenda shule moja. Mkuu wa mkoa washa gari, tukaenda. Mwalimu akashangaa tunaingia tu vuuu, tukamwambia tunaomba tukaone choo cha wanafunzi, baadaye tukasema tunataka tuongee na wanafunzi, tukauliza wangapi hapa wana kitanda kimoja kimoja... nikasema kweli, nikikuta kuna shida na wewe mdhibiti ubora upo nitajua uliajiriwa kwa undugu.

"Kuna Mkuu wa Wilaya ambaye ni kiongozi wa mambo yote taarifa imfikie kwenye shule yako hapa kuna mwalimu mkuu ameingiza wanafunzi wengi kuliko vitanda, hawa wanalala pamoja tunakuza maadili gani? Na wazazi wanajua hilo?

"Kuna shule moja nilienda mimi na dereva tu na nilitonywa, nikaenda nikauliza 'mwalimu mkuu yupo wapi?'

"Mimi ni Waziri wa Elimu akasema, 'ooh karibu ofisini' nikamwambia 'hapana twende kwenye choo', nikakuta matundu mawili wanafunzi 600.

"Nikamtuma Kamishna wa Elimu maana nilimwambia mkurugenzi akasema anashughulikia, bila kujua tulirudi tena na ile siku ndio tulikuwa tunafunga ile shule lakini ndani ya wiki choo kilijengwa kikaisha kwenye jiji," alisema.

Waziri huyo alisema hawawezi kuruhusu shule iwe na mazingira yanayoondoa malezi na uadilifu, na ameagiza ripoti zianze na Mkoa wa Dodoma kwa kuwa ni makao makuu.

Aliagiza kupewa ripoti kuhusu hali ya vyoo kwa kuwa ni muhimu kwa wasichana ili wasiache shule na kuwataka wadhibiti hao kuhakikisha shule zinatenga fedha za kujenga vyoo.

"Sisi Rombo tunakwenda vizuri, tunashawishi waliosoma shule hizo wakati wa Krismasi watumie kwenda kuangalia shule walizosoma zikoje, imetusaidia sana vyoo vingi vimejengwa na wananchi Rombo," alisema.

**UWIANO DARASANI**

Waziri huyo alisema: "Hivi Kasulu wastani wa wanafunzi kwa mwalimu mmoja ni 104, inamaana kuna sehemu wanafunzi ni zaidi ya 104 kwa mwalimu mmoja na wengine ni kidogo na mdhibiti ubora yupo pale, anasema 'nimeshaandika ripoti yangu na nimemaliza kazi yangu'.

"Hapo ulipo Tanzania hii ni moja, mtoto anayesoma Kinondoni wastani wa mwalimu mmoja ni wanafunzi 31, kwa hiyo kuna nafasi kubwa ya mwalimu kumhudumia mwanafunzi na kumsikiliza na kuona changamoto zake, huyu mtoto wa Kinondoni ni Mtanzania na wa Kasulu ni Mtanzania na tunajenga taifa la watu walio sawa.

"Tulipopeleka fursa hizi kwa haki na usawa kwenye nchi hii hatuwatendei haki watu wengine. Arusha Mjini tulikuwa kule juzi, mkuu wa wilaya anasema sisi Arusha tumekuwa wa kwanza, walimu wamerundikana pale, anayesoma pale ni Mtanzania na anayesoma Uyui ni mtanzania, mdhibiti ubora yupo, anasema 'nimeshajaza ripoti yangu nimeshamaliza'."

Aliwataka watendaji hao kupiga kelele ili walimu watoke mijini wakafundishe vijijini.

"Shule inavuja, mdhibiti ubora upo, watoto mvua ikinyesha wanasomaje? Mkurugenzi wa Halmashauri kwanini atumie fedha kwenye kitu kingine?" alihoji.

Prof. Mkenda alisema kwenye elimu kuna mambo matatu yanazungumzwa ikiwamo ubora wa elimu, elimu iakisi mahitaji yaliyopo na suala la malezi.

Alifafanua kuwa anasikia na anaona kwenye mitandao ya kijamii mambo mengi yanatokea ya ovyo kutokana na tatizo la malezi.

Alisema watoto wanapaswa kulelewa kwenye mazingira ya kukuza utamaduni na maadili ya nchi.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Prof. James Mdoe, alisema bila elimu msingi iliyo bora, ngazi zingine zote zitakuwa ngumu katika kudhibiti ubora ipasavyo na kuwasihi kuongeza weledi kwa ajili ya kazi hiyo.

Mkurugenzi wa Idara ya Udhibiti Ubora wa Shule wa Wizara hiyo, Euphrasia Buchumu, alisema katika kikao hicho watapitia mwongozo wa usajili wa shule ili kuhakikisha utoaji wa elimu unafuata sera sheria, kanuni, nyaraka na miongozo ya wizara.

Kamishna wa Elimu nchini, Dk. Lyabwene Mtahabwa, aliwataka wadhibiti ubora wa elimu hao kuwa viongozi bora ambao watu watawafuata badala ya kuwakimbia.

## Rais Samia azitaka benki zishushe riba

**Na Richard Makore,** MISENYI

RAIS Samia Suluhu Hassan amezitaka benki nchini kushusha riba chini ya asilimia tisa katika mikopo kwa sekta ya kilimo ili kuwasaidia wakulima kuongeza uzalishaji.

Ameagiza Benki Kuu ya Tanzania (BoT) kukaa pamoja na benki hizo ili kutekeleza suala hilo kwa lengo la kuwasaidia wakulima wanaohitaji mikopo.

Alitoa agizo hilo jana wilayani Misenyi mkoani Kagera alipotembelea Kiwanda cha Sukari cha Kagera.

Rais Samia alisema wakati wa benki kushusha riba zaidi kuliko ilivyo sasa kwa wakulima umefika ili kukuza sekta ya kilimo.

"Ninafahamu CRDB inatoza riba ya asilimia tisa, lakini nyingine bado zipo juu, ninaomba serikali kupitia BoT tutakaa na hizi benki kuona namna ya kushusha hii riba katika mikopo kwa sekta ya kilimo," aliagiza.

Akizungumza na wafanyakazi na uongozi wa kiwanda hicho, Rais Samia aliwapongeza kwa uwekezaji walioufanya.

Alisema kuwa miaka 50 ijayo biashara nyingi zitategemea mazao ya kilimo na Tanzania kama nchi ni lazima kuanza kuchukua hatua za kukuza sekta hiyo.

Aliongeza kuwa bado kuna upungufu wa sukari nchini na kiwanda hicho kihakikishe kinazalisha kama kilivyojiwekea malengo yake ili kutatua tatizo hilo. Aliahidi kuendelea kulinda wawekezaji wote nchini kwa kuwa wana mchango mkubwa katika kukuza uchumi wa nchi.

Katika kuunga mkono uwekezaji uliofanywa na kiwanda hicho, Rais Samia alikubali kutoa ardhi ya Gereza la Kitengule lililoko wilayani Karagwe mkoani Kagera kwa sharti la kuwauzia.

"Nimekubali kuwapatia ardhi hiyo mfanye upanuzi wa mashamba ya miwa kwa ajili ya kuzalisha sukari, lakini kwa sharti la kuwauzia," alisema.

Awali, Mwenyekiti wa Bodi ya kiwanda hicho, Seif Ali Seif, aliomba kupatiwa eneo linalomilikiwa na gereza hilo ili waongeze uzalishaji.

Alisema kiwanda hicho kitaendelea na upanuzi ili kuzalisha sukari ya kutosheleza mahitaji ya bidhaa hiyo nchini. Akizungumza katika kiwanda hicho, Waziri wa Kilimo, Husein Bashe, alisema kwa sasa nchi inaagiza tani 210,000 kutoka nje ili kukidhi mahitaji ya ndani.

Aliagiza kiwanda hicho kuanza kuzalisha tani 390,000 hadi tani 400,000, huku akitaka sukari kwa ajili ya matumizi ya viwandani ianze kuzalishwa nchini badala ya kuendelea kuagizwa nje.

Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji, alisema kwa mwaka uzalishaji wa sukari nchini ni tani 468,863.

Alisema kuna upungufu wa asilimia 100 wa uzalishaji wa sukari za viwandani na kwamba serikali inaweka juhudi ili kumaliza tatizo hilo.

Katika ziara yake hiyo, Rais Samia pia aliagiza serikali kuzikopesha Sh. milioni 500 bodi za mamlaka za maji ili kusaidia kuwavutia maji wananchi wanaozunguka miradi mbalimbali.


Dev Recoveries Ltd

NIC Life House 4th Floor, Wing C
Sokoine Drive/Ohio Street
P. O. Box 6100
Dar es Salaam
Tel:+255 22 2112045
Fax: +255 22 2112045
info@transmark-tz.com
www.transmark-tz.com

**MARUDIO YA MNADA WA HADHARA**
**NOTISI YA KULIPA DENI NA MNADA WA HADHARA**

Kampuni ya Dev Recoveries Limited kwa idhini tuliyopewa na **EQUITY BANK TANZANIA LIMITED,** tunatangaza marudio ya **MNADA WA HADHARA**, Mnada utafanyika kuanzia saa 4:30 asubuhi na kuendelea mahali dhamana ilipo kama inavyoonyesha hapa chini.

| NA | JINA LA MDAIWA | DHAMANA/MAHALI ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|
| 1 | SOBAI ASANJA LIMITED | Hati Na. 38083/159, Kiwanja No.63/27 Upanga, Dar es Salaam City | 21/06/2022 Kuanzia saa 04;30 asubuhi |
| 2 | SOBAI ASANJA LIMITED | Hati Na.38083/150, Kiwanja Na.63/27 Upanga Dar es Salaam City | 21/06/2022 Kuanzia saa 04;30 asubuhi |
| 3 | SOBAI ASANJA LIMITED | Hati Na.38083/151, Kiwanja Na.63/27 Upanga Dar es Salaam City | 21/06/2022 Kuanzia saa 04;30 asubuhi |
| 04 | SOBAI ASANJA LIMITED | Hati Na.38083/167, Kiwanja Na.63/27 Upanga Dar es Salaam City | 21/06/2022 Kuanzia saa 04;30 asubuhi |

116896202

**MASHARTI YA MNADA**
1. Dhamana itauzwa "kama ilivyo".
2. Mnunuzi atatakiwa kulipia 25% ya bei ya mnada siku ya mnada na kiasi cha pesa kilichobaki kilipwe kama watakavyokubaliana malipo hayo yaliyobakia baina ya benki na mnunuzi.
3. Gharama za kubadilisha hati miliki (transfer of ownership) na gharama nyingine ni za mnunuzi.
4. Ukaguzi wa dhamana utafanyika kuanzia siku ya tangazo hili kutoka kuanzia saa 4:00 asubuhi na kuendelea.
5. Kwa mawasiliano zaidi piga namba za **simu 0782 065 914 / 0712 073 682**

# Waziri Mkuu: Serikali haitavuna wanyamapori

**Na Salome Kitomari,** DODOMA

SERIKALI imesema haikusudii kuvuna wanyamapori wakiwamo tembo ambao wameongezeka, badala yake inafanya tathmini na kuchukua hatua za kuzuia madhara kwa binadamu na mali zao.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alitoa kauli hilo jana bungeni jijini hapo wakati akijibu maswali ya papo kwa papo ya wabunge.

Katika swali lake, Mbunge wa Mlalo, Rashid Shangazi, alitaka kujua mpango wa serikali kuwahakikishia wananchi walioathiriwa na wanyamapori kama tembo wasiendelee kupata athari za mali na maisha yao. Alisema suala la ulinzi wa mali na usalama wa raia ni jukumu la serikali na kwamba ongezeko la wanyama wakali kama tembo ambao wanavamia maeneo yaliyoko pembezoni mwa hifadhi za taifa na mapori tengefu kwa nyakati tofauti linaathiri shughuli za kijamii, kiuchumi na kusababisha vifo vya watu.

Waziri Mkuu akijibu swali hilo, alisema zipo jitihada za serikali kupunguza au kumaliza kabisa madhara kwenye maeneo ya pembezoni mwa hifadhi huku akitaja baadhi ya maeneo aliyotembelea na kujionea uharibifu kuwa ni Mlalo, Kilwa, Lindi Vijijini na Liwale, Tunduru, Meatu, Bariadi na Serengeti na kilio kikubwa ni ongezeko la tembo.

"Jitihada zilizofanyika ni kuongeza idadi askari wa wanyamapori wanaopelekwa kwenye hifadhi zinazopakana na makazi ya watu.

"Pia kujenga vituo 32 vya kutunza silaha za kuwaondoa warudi kwenye maeneo yao, pale Rondo mkoani Lindi kulikuwa kituo cha maliasili cha kupunguza wanyama wakali wanaoingia kwenye makazi ya watu mkoani humo, tutakiboresha na kuweka silaha na askari ili kusaidia wananchi," alisema. Kwa mujibu wa Waziri Mkuu, wanyamapori, hasa tembo licha ya ongezeko lao, serikali haikusudii kuvuna bali kuzuia kuingia kwenye makazi ya watu. "Tembo yuko kwenye tano bora ya wanyama tunaotakiwa kuwahifadhi kama nyara ya taifa. Serikali kwa namna yoyote ile itaendelea kuwahifadhi, waendelee kuwa tunu ya taifa letu.

"Niwahakikishie wananchi wanaoishi pembezoni wameendelee kupata tatizo kuwa mkakati wa askari unaendelea, tumewakabidhi Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA) kusimamia kwa karibu," alisema.

"Tutaendelea kufanya tathmini, kuimarisha mifumo ya wanyama hawa, ili kupunguza madhara ya wanyama hao kwa binadamu na mali zao ili watu waishi kwa amani," alisema.

# Bunge laipa serikali miezi 3 majibu mauaji hifadhini

**Na Salome Kitomari,** DODOMA

SPIKA wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, ametoa miezi mitatu kwa serikali kuwasilisha bungeni taarifa ya uchunguzi na tathmini ya uharibifu wa mali na vifo vya wananchi vilivyotokana na wanyamapori au uhifadhi kwa ujumla.

Kiongozi huyo alilazimika kutoa uamuzi huo jana bungeni jijini hapa kutokana na Mbunge wa Tarime Vijijini, Mwita Waitara na Mbunge wa Songwe, Philipo Mulugo, Juni 3 mwaka huu kudai kuna wananchi 90 wameuawa, kujeruhiwa na kuharibwa mali zao kutokana na uwapo wa hifadhi za taifa. Wabunge hao kwa nyakati tofauti walitakiwa kupeleka ushahidi kwa Spika kuhusu madai yao hayo kwa mujibu wa sheria na walipopeleka, Spika alisema haukuwa ushahidi wa kuonyesha namna uwapo wa hifadhi umesababisha vifo, majeruhi na uharibifu huo.

"Baada ya wabunge hawa kuwasilisha ushahidi wao kwangu, nimeona niwasilishe serikalini ili ifanye uchunguzi wa kutosha na kwa wakati mwafaka ndani ya miezi mitatu, Bunge lipate taarifa juu ya uhalisia wa jambo hili," alisema Spika.

Wakati wakichangia hoja ya Waziri wa Maliasili na Utalii, Mwita alisema bungeni kuwa kuna watu 10 wameuawa jimboni kwake kutokana na uwapo wa Hifadhi ya Taifa Serengeti.

Mbunge Mulugo alitakiwa kuwasilisha orodha ya watu 80 aliodai bungeni kwamba wamepoteza maisha kutokana na kuuliwa na wanyama, uharibifu wa mazao na ulemavu dhidi ya tembo, simba na mamba kutoka mwaka 2016 hadi 2022.

"Nawajulisha kuwa wabunge husika walileta mawasilisho hadi Juni 8, mwaka huu, niliyafanyia uchambuzi nilibaini walichowasilisha ni yale yale malalamiko ya wananchi wakati wakichangia hoja bungeni, hawajaleta uthibitisho," Spika alisema.

Alibainisha kuwa Mwita aliwasilisha majina ya wananchi na kuambatanisha picha za wananchi hao zikionekana kuwa na athari mbalimbali ikiwamo ulemavu wa miguu, alama za vidonda na kuashiria kwamba walipata athari kutokana na hifadhi hiyo, ikiwamo kupigwa.

"Huu siyo ushahidi wa kuonyesha madhara haya yanatokana na hifadhi au shughuli za askari wanyamapori," alisema.

Spika Tulia alisema Mulugo aliwasilisha orodha ya wananchi 87 anaodai walipata madhara mbalimbali, ikiwamo vifo na kuharibiwa mazao yao na wanyamapori bila kutoa ushahidi wa wazi namna wananchi hao walivyoathiriwa na wanyama hao.

"Pamoja na kwamba hakuna uthibitisho wa wazi uliowasilishwa, ni wazi kuwa moja ya majukumu ya kikatiba ya Bunge, hiki ni chombo cha wananchi cha kupokea malalamiko yao kwa njia mbalimbali, ikiwamo wawakilishi wao ili serikali iyafanyie kazi."Kwa kuzingatia muktadha wa malalamiko hayo na athari zake kwa wananchi na kwa kuwa Bunge halina uwezo wa kuthibitisha kuwa matukio hayo na athari zinatokana na uwapo wa wanyamapori au hifadhi ama yamesababishwa na askari wanyamapori, nimeona ni vyema niwasilishe serikalini," aliagiza.

Spika aliwataka wabunge kuzingatia kanuni wanapochangia hasa mambo wanayoyasema kuhusu wananchi na kwa jambo ambalo mbunge hana uhakika, aliseme kwa namna ambayo hana uhakika na serikali italifuatilia kuliko kuonyesha ana uhakika.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**MANISPAA YA MPANDA**

Simu Na. 255-252957128
Nukushi: 255-252957129
Barua pepe: md@mpandamc.go.tz

Ofisi ya Mkurugenzi,
Halmashauri ya Manispaa,
S. L. P 216,
MPANDA.
Tarehe: 10/06/2022

## TANGAZO LA MNADA WA KUUZA MALI CHAKAVU ZA HALMASHAURI

Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda inakusudia kuuza magari, pikipiki, trekta na trela kwa mnada wa hadhara kama ifuatavyo;-

### A. MAGARI

| S/N | LOT NO. | Namba ya Usajili | AINA YA GARI | Chasis NO. | ENGINE NO. | SEHEMU ILIKO |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | MMC/MV/TATA/2020/21/01 | STH 245 | TATA | 3490732-80888 | 697D012-88601 | SHULE YA SEKONDARI YA |
| 2 | MMC/MV/ISZ/2020/21/04 | STG 1634 | ISUZU LORY | 1686483 | 866860 | SHULE YA SEKONDARI MWANGAZA |

### B. PIKIPIKI

| S/N | LOT NO. | Namba ya Usajili | AINA YA PIKIPIKI | Chasis NO. | ENGINE NO. | SEHEMU ILIKO |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | MMC/MC/2020/21/06 | STK5483 | YAMAHA | 3GX-100134 | 3GX-099874 | OFISI YA MANISPAA MPANDA |
| 2 | MMC/MC/2020/21/07 | STK5497 | YAMAHA | 3GX-100142 | 3GX-099888 | OFISI YA MANISPAA MPANDA |
| 3 | MMC/MC/2020/21/08 | STK5430 | YAMAHA | 3GX-100316 | 3GX-100557 | OFISI YA MANISPAA MPANDA |
| 4 | MMC/MC/2020/21/09 | STK5504 | YAMAHA | 3GX-100153 | 3GX-099909 | OFISI YA MANISPAA MPANDA |

### C. TREKTA

| S/N | LOT NO. | Namba ya Usajili | AINA | Chasis NO. | ENGINE NO. | SEHEMU ILIKO |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | MMC/PLT/2020/21/02 | | TRACTOR KUBOTA | L345-II-10168 | - | SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA MPANDA |

### D. TRELA

| S/N | LOT NO. | Namba ya Usajili | AINA | Chasis NO. | ENGINE NO. | SEHEMU ILIKO |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | MMC/TL/2020/21/03 | | TRELA | - | - | SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA MPANDA |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Mnunuzi atalipa asilimia 25% ya bei iliyofikiwa papo hapo baada ya nyundo ya dalali kushuka na kiasi cha 75% kilichobaki kitalipwa ndani ya siku 14 (kumi na nne) baada ya siku ya mnada. Atakayeshindwa kulipa hiyo asilimia 75% katika muda huo ushindi wake utafutwa na hatarudishiwa kiasi alichotanguliza na mali hiyo itanadishwa tena.
2. Ukaguzi wa magari,pikipiki,trekta na trela utafanyika siku tatu kabla ya mnada kuanzia saa 4.00 asubuhi hadi saa 8 mchana.
3. Gharama zote pamoja na usafiri,malazi, ukaguzi na kuhamisha umiliki wa mali ni juu ya mnunuzi mwenyewe.
4. Magari,Pikipiki,Trekta naTrela yatauzwa kama yalivyo na jinsi yanavyoonekana.
5. Ikumbukwe kuwa Magari, Pikipiki, Trekta na Trela hayajalipiwa kodi. Ni wajibu wa mnunuzi kulipa kodi husika za Serikali.
6. Mnada utafanyika Siku ya Alhamisi tarehe 23/06/2022 kuanzia saa 3:00 asubuhi katika eneo la Ofisi ya Mkurugenzi Makao Makuu yaliyopo Ilembo, Shule ya Sekondari Mwangaza na Shule ya Sekondari ya Wasichana Mpanda.

**MKURUGENZI WA MANISPAA MPANDA.**

216895101

# Washikiliwa polisi tuhuma za uhalifu, wamo watoto

**Na Friday Simbaya,** IRINGA

JESHI la Polisi mkoani Iringa limewakamata watuhumiwa 21 wa makosa mbalimbali ikiwamo uvunjaji na wizi, wakiwamo 10 ambao ni watoto.

Limesema kuwa watoto hao walikamtwa walipokuwa wanazagaa ndani ya Manispaa ya Iringa pasi na kuwa na makazi maalum.

Akizungumza na waandishi wa habari mkoani Iringa jana, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Iringa, Allan Bukumbi, alisema jeshi hilo katika mikakati ya kuimarisha ulinzi na usalama, linaendelea kufanya doria na misako mbalimbali ya kupambana na uhalifu.

Alisema kuwa watoto waliokamatwa, kwa sasa wako chini ya uangalizi wa Jeshi la Polisi na kinachoendelea ni kukamilisha taratibu za kuwarudisha nyumbani kwa wazazi na walezi wao.

Kamanda Bukumbi alitaja majina ya watoto wenye umri wa kuanzia miaka 11 hadi 17, lakini kutokana na sababu za kisheria, Nipashe haitaanika majina hayo.

Aliongeza kuwa mbali na watoto hao, jeshi hilo pia linawashikilia wazazi wanane kwa tuhuma za kutelekeza na kushindwa kutoa malezi bora na elimu kwa watoto, hivyo kusababisha watoto kuzagaa ovyo mtaani na upelelezi ukikamilika wazazi hao watafikishwa mahakamani.

Kiongozi huyo wa Jeshi la Polisi alikumbusha kuwa mzazi kumlea mtoto ni wajibu wa kisheria na kushindwa kumtunza na kumtelekeza mtoto ni kosa la jinai.

Kamanda Bukumbi alisema jeshi hilo pia limemkamata Enock Abraham (20), raia wa Ethiopia na wenzake wanne kwa tuhuma za kuingia nchini bila kibali.

Alisema kuwa Juni 7, mwaka huu, majira ya saa nne usiku, huko maeneo ya Ruaha Mbuyuni Darajani, Kata ya Ruahambuyni, Tarafa ya Mahenge wilayani Iringa, askari wakiwa kazini eneo la kizuizi cha magari, walipata taarifa kutoka kwa raia wema kuwa kuna watu wamejificha porini.

Kamanda Bukumbi alisema kuwa walipokwenda porini walimkuta Abraham na wenzake wanne na walipofanyiwa mahojiano, walidai wameshushwa na gari maeneo hayo ili wapumzike baada ya safari ndefu.

Alisema kuwa raia hao walikuwa kuwa kwenye gari wasilolikumbuka ambalo liliwabeba kutoka Nairobi, Kenya kuelekea Afrika Kusini walikodai kwamba walikuwa wanakwenda kutafuta maisha.

Kamanda Bukumbi alisema raia hao wa kigeni wanashikiliwa na polisi na watafikishwa mahakamani pindi taratibu zitakapokamilika.



Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Reja Reja wa Benki ya I&M, Lilian Mtali (kulia), akijaribu kumvalisha kifaa cha kusikia mwanafunzi wa darasa la nne wa shule ya Msingi ya Mtoni, Abdul Juma, baada ya benki hiyo kutoa msaada wa madawati 100 pamoja na vifaa vya usikivu 50 kwa shule hiyo, wilayani Temeke, mkoani Dar es Salaam juzi, ikiwa ni juhudi za kuunga mkono serikali kuhakikisha kuwa wanafunzi wanapata elimu kwenye mazingira bora na rafiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waiahidi mahakama kuacha tabia mbaya

**Na Grace Gurisha**

ALIYEWAHI kushiriki mashindano ya Miss Tanzania mwaka 2020, Rashida Wanjara na wenzake 13, wameiahidi Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu kuwa hawatacheza tena 'kibao kata' wala kutumia chupa na tango kwa kipindi kisichopungua miaka miwili na pia watabadilika tabia zao mbaya.

Washtakiwa hao akiwamo Masha Ngubi 'Masha Love' walifikia uamuzi huo baada ya Jamhuri kuwasilisha maombi mahakamani hapo ya kuwataka washtakiwa hao waiahidi mahakama kuwa watabadilika na kuwa na tabia njema.

Wakati anatoa uamuzi wa maombi hayo, Hakimu Tarimo alisema kila mshtakiwa anatakiwa kuwa na wadhamini wawili waliotakiwa kutia saini bondi ya Sh. milioni tano na pia aliwataka wawe na nidhamu na tabia njema katika jamii.

Hakimu Tarimo pia aliwataka washtakiwa kutokufanya makosa yoyote ya kimaadili na watatakiwa kuripoti kwa Mkuu wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai Kanda (ZDCO) mara moja kwa mwezi.

Alisema ikifika mwakani mwezi Juni, washtakiwa watatakiwa kuripoti kwa mkuu huyo mara moja kwa miezi mitatu na kuwataka wawe mabalozi wazuri na waende wakawabadilishe wengine katika jamii.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Janeth Magoho, alidai jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Rita Tarimo, kuwa wameleta maombi maalum ya washtakiwa 14 ambao wanatakiwa waahidi mbele ya mahakama kuwa watakuwa na tabia njema kwa muda usiopungua miaka miwili.

Pia alidai washtakiwa waahidi kuwa hawatafanya kosa lolote la jinai ambalo linahusika na utu wa binadamu na pia mahakama inaweza kutoa amri yoyote itakayoona inafaa.

Alidai maombi hayo yameungwa mkono na kiapo cha ACP Faustine Mafwele kutoka Ofisi ya Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai (DCI), akiomba mahakama ipokee maombi hayo ili washtakiwa waiahidi mahakama.

Baada ya Magoho kuwasilisha maombi hayo, Wakili wa Wajibu Maombi, Ruben Semwanza, alidai hawana pingamizi na maombi ya Upande wa Jamhuri.

Pia alidai washtakiwa wamekaa mahabusu kwa muda tofauti tofauti, hivyo kuiomba mahakama itoe masharti nafuu ili washtakiwa wawe huru na kama kuna tija ya kuleta kiapo kinzani watakiwasilisha.

Wakili Abiati Sivea aliiomba mahakama itoe adhabu ndogo kwa washtakiwa kwa kuwa wana umri mdogo na wanawategemea wazazi wao na ni wanafunzi.

Baada ya mawakili hao kuiomba Mahakama, Hakimu Tarimo alianza kuwauliza mshtakiwa mmojammoja kama wanakubaliana na ombi la Jamhuri la kubadilika kimaadili kwa kuiahidi mahakama.

Kila mmoja kwa nafasi yake aliahidi kuwa balozi mzuri katika nchi, atakuwa mwadilifu, atajirekebisha tabia na pia hatarudia kufanya tabia mbaya.

Baada ya washtakiwa kuiahidi mahakama, Hakimu Tarimo alirejea kwenye kiapo cha ACP Mafwele na kueleza kuwa kiapo hicho kinaeleza kuwa wanacheza 'kibao kata', kwa hiyo waache na hiyo tabia.

Hakimu Tarimo pia aliieleza kwamba waache kutumia chupa, tango na vitu vingine vinavyofanana kama hivyo, ambapo washtakiwa waliiahidi mahakama kuwa wanaacha mambo hayo.

Mbali na Wanjara na Masha love, washtakiwa wengine ni Rhodie Webb, Hawa Anthony, Lydia Mlelwa, Malkia Hashim, Latifa Idd, Mariam Bakari, Hadija Said, Zena Abdallah 'Jikeshupa', Mariam Idd, Nasra Kondo, Irene John na Joyce Matulanga.

# NBC yaweka kambi kaskazini kuamsha sekta za utalii, kilimo

**Na John Badi**

BENKI ya Taifa ya Biashara (NBC) imeelezea dhamira yake ya kukuza na kuchochea ukuaji wa kiuchumi katika mikoa ya Kanda ya Kaskazini kwa kuunga mkono jitihada zinazofanywa na serikali katika kukuza sekta za utalii, kilimo, ufugaji na biashara.

Katika kuthibitisha dhamira yake hiyo, viongozi waandamizi wa benki hiyo wakiwamo wawakilishi wa bodi ya wakurugenzi, wakurugenzi na wakuu wa idara mbalimbali wa benki hiyo mwishoni mwa wiki walitembelea mikoa ya Manyara, Arusha na Karatu wakilenga kukutana na wateja wao katika sekta hizo, ili kwa pamoja wajadili fursa za kibiashara, mipango ya ukuaji na huduma mpya zitolewazo na benki hiyo.

Akizungumza kuhusu matukio hayo, Mkurugenzi wa Kitengo cha Biashara kwa Wateja Binafsi NBC, Elibariki Masuke, alisema kupitia hatua hiyo wamekutana na wateja wao na kupata wasaa wa kutambulisha huduma zao mpya sambamba na kupokea mrejesho kuhusu mahitaji ya wateja wao hususani kipindi hiki ambacho mikoa hiyo ipo kwenye mkakati wa kuboresha zaidi sekta ya utalii. "Rais wetu na serikali kwa ujumla wamefanya jitihada kubwa katika kuinua sekta ya utalii na hivyo sisi kama wadau muhimu kwenye hilo tumeona tuje kumuunga mkono kufanikisha adhima yake hiyo.

"Kupitia huduma yetu ya NBC Biashara Club tumeweza kukutana na walengwa ambao ni wateja wetu na tumeweza kujadili na kuwasilisha huduma zetu mpya zinazoendana na dhamira hii kuu ya kukuza utalii ikiwamo huduma yetu ya mikopo ya magari ya utalii huku dhamana ikiwa ni magari yenyewe," alisema.

Alitaja huduma nyingine kuwa ni pamoja na huduma ya mikopo ya zana za kilimo yakiwamo matrekta huku dhamana ikiwa ni kifaa chenyewe, mikopo ya wazabuni pamoja na mikopo ya wafanyabiashara wanaonza biashara inayofahamika kama 'NBC Kua Nasi'.

Mkurugenzi wa Kitengo cha Biashara kwa Wateja Wadogo na wa Kati wa NBC, Elvis Ndunguru, alisema kupitia dhamira hiyo, benki hiyo inatarajia kuboresha zaidi huduma yake ya malipo ya POS ili kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato yakiwamo ya fedha za kigeni.

"Sekta ya utalii inachangia zaidi ya asilimia 25 ya fedha za kigeni. Kwa hiyo, uboreshaji wa mfumo wa ukusanyaji wa mapato ni muhimu sana, hivyo mwisho mwa mwezi huu tunatarajia kuzindua huduma yetu ya POS iliyoboreshwa zaidi kwa ajili ya malipo ya dola na shilingi.

"Pia tunatarajia kuongeza huduma ya American Express kwenye mfumo huo ili kuhudumia pia wateja wa Marekani," alisema. Mkuu wa Mkoa wa Arusha, John Mongella, alisema hatua hiyo imechukuliwa wakati mwafaka kwa kuwa kupitia jitihada za Rais Samia Suluhu na serikali za kuboresha sekta ya utalii nchini, ukanda huo unatarajia kupokea watalii wengi zaidi mwaka huu, hivyo maboresho zaidi katika huduma za kifedha ni muhimu.

"Kwa mfano, mkoa wetu wa Arusha tunategemea utalii kwa asilimia 80. Tayari Rais ameshafanya jitihada nyingi za kufanikisha ukuaji wa sekta ya utalii, kilichobaki ni sisi viongozi na wadau wengine kumuunga mkono kama wanavyofanya NBC kwa sasa.

"Tunaamini jitihada zao hizi mbali na sekta ya utalii tutaona mabadiliko makubwa katika sekta za kilimo, biashara na ufugaji pia... tunawashukuru sana," alipongeza.

Akiishukuru benki hiyo kwa niaba ya wateja wote, Mhandisi Matoleo Ouden ambaye ni mfanyabiashara jijini Arusha, alisema kupitia ujio wa viongozi hao waandamizi, wamepata wasaa wa kuwasilisha mahitaji yao kwa viongozi waandamizi wa benki hiyo ili yafanyiwe kazi na uamuzi kutoka ngazi ya juu.

# Tangazo kwa Umma

**ASSA ABLOY** imejidhatiti kutoa bidhaa zenye ubora wa hali ya juu kwa wateja wake ndani ya nchi ya Tanzania. Mteja anayenunua Bidhaa za **ASSA ABLOY** anafanya hivyo akiwa na imani na ubora unaotokana na uhakika wa bidhaa.

Kwa wiki kadhaa zilizopita, **ASSA ABLOY** imekuwa ikifanya kazi na Tume ya Ushindani ya Tanzania kupunguza bidhaa zisizo halisi ambazo zina nembo ya **ASSA ABLOY** isivyo halali.

Ili kuhakikisha kwamba mteja analindwa, **ASSA ABLOY** itaendelea kufanya ukaguzi/uchunguzi huo mara kwa mara. Nembo za **ASSA ABLOY** kama vile **UNION na YALE** zinaongoza na Kuhaminika kwenye majengo ya kibiashara na makazi ndani ya Tanzania.

Tunawasisitiza wateja wetu wote wa Jumla na reja reja kununua bidhaa za **ASSA ABLOY** kutoka kwa wazambazaji na Washirika wetu walioidhinishwa tu. **NEW TAHERY STORES (1989) LTD** ni mmoja wa wasambazaji na washirika wetu wahaminifu ndani Tanzania.

## KATAA BIDHAA FEKI

216892902

ASSA ABLOY

**Ikishirikiana na**

NTS Since 1989 NEW TAHERY STORES (1989) LTD

+30 Years of Experience Delivering Original ASSA ABLOY Products in TZ

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Hili la utapeli 'kamari mtandao' liandaliwe vita vipya kulimaliza

**KUNA** jambo linalotoa maswali mengi ya kijamii sasa. Mambo yote yana majibu kwa umma, iwe kisheria au hata kutumia kanuni kadhaa za kiserikali, lakini kasoro zake hazikomi.

Swali la utapeli kwa michezo ya kubahatisha kupitia mifumo ya mitandao na hasa simu za mkononi linaendelea kuumiza watu. Siku chache zilizopita, kundi kubwa la kijamii limeumizwa kupitia michezo ya kubahatisha yenye kanuni zake, ikielezwa mtu anawekeza kiasi fulani cha fedha kutarajia faida na ndipo anaangukia kidevu.

Tahadhari nyingi zimeshatolewa na serikali kuwataka watu wawe makini na haya, lakini kama vile kumpigia mbuzi gitaa. Maana aina hiyo mpya ya utapeli mara tu baada ya kujitokeza kwenye mtandao, huku mmiliki wake halisi haeleweki sawa, wakakurupukia kuamini wanawekeza fedha kwenye kamari hiyo wavune, lakini wanaangukia kuvunwa na matapeli.

Ingawa kundi kubwa linaficha kiasi cha dhuluma, imebainika kiwango cha dhuluma kwa wengi ni kati ya Sh. 20,000 na Sh. milioni mbili. Ni aina ya dhuluma inayofanana sana na kilichotokea huko nyuma katika mchezo wa kubahatisha usio rasmi, kwa kivuli cha kampuni ya DECI. Wengi walitaharuki na kukimbilia kujiunga kucheza kamali hiyo yenye matarajio wangevuna pesa, ila wakaishia kuvunwa kiasi kikubwa cha pesa.

Tunakumbuka baada ya mkasa wa watu kutapeliwa kupitia kamali ya DECI ambayo taharuki yake ilituma salamu kwa wengi, serikali nayo ikichukua hatua za kuimarisha kanuni na sheria husika, bado inaonekana kuna shida ambayo inaacha maswali, shida iko wapi, uelewa au kiburi cha wanaojitosa kucheza katika mazingira hayo kama ya sasa.

Msingi wa michezo ya kubahatisha nchini ina sheria yake mamlaka maalum, Bodi ya Michezo ya Kubahatisha inayosajili na kusimamia michezo, pia kusimama vigezo na haki zote za kisheria kwa wachezaji na wachezeshaji, hata serikali katika nafasi yake ikiwamo kodi. Hapo ndipo inazaa swali, shida imekaa wapi?

Baada ya mkasa ambao hadi mwanzoni mwa wiki hii, kumeshuhudiwa vilio vya kutapeliwa, Nipashe ilipochukua hatua ya kiudadisi undani, si Benki Kuu (BoT) au wizara husika, zote zimekana kuutambua mchezo huo na kuuacha kando kuwa utapeli. Hapo napo kunahalalisha kwamba wanaocheza kudhulumiwa tena na 'mtu asiyejulikana.'

Hatua hiyo ilijidhihirisha zaidi, pale wachezaji hasa waliojihusisha na mtandao huo wakiwekeza fedha zao zisizorudi, wakaanza kukatishwa tamaa mtandaoni, wakipewa kauli zenye ishara za kutapeliwa kwao.


Ni aina ya ujumbe wa kimtandao ambao wachezaji wake awali wanasema ilikuwa tofauti, kwani walipewa kauli za hamasa kibiashara. Ghafla zikatoweka, baada tu ya kubainika na kuwapo kauli ya umma kwamba kunafanyika utapeli katika mtandao huo, ikisambaa hadi katika vyombo vya habari.

Kwa majumuisho ya yote inaonekana kuna shida bado katika haki kupitia ndani ya mifumo ya mitandao ya jamii. Kuna suala la uelewa kuhusu mitandao, sheria zake na mantiki ya kielimu kwa jumla, huku kukiwapo wanaotaka kupata kipato kwa njia za mkato.

Tunajua serikali imefanya juhudi za makusudi katika kukabili madhila ya yanayojificha katika mifumo ya mitandao ya jamii, pia michezo ya kubahatisha kwa sheria, miongozo na vyombo maalum vinavyosimamia.

Ila kwa hili tunaloshuhudia tena, bado kuna mambo makuu mawili yanayostahili serikali kuchukuwa hatua zaidi. Kwanza, elimu zaidi kwa umma inatakiwa maana kuna kiashiria cha upungufu katika uelewa, pia wahusika wa utapeli wasakwe kwa nguvu zote kwa kutumia mamlaka za usalama wa dola, maana kinachojengwa si sahihi na tusishangae, DECI nyingine ikajirudia kama hapatakuwapo udhibiti sahihi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Florida Raymond, TUDARCo

## Muungwana Lazima Nilonge

# Mfumo majitaka Mwenge Mlalakuwa una sababu zote za kufanyiwa kazi

**NI** kawaida kwa serikali zote duniani, kwamba huwa zinatafuta mbinu mpya za kugharimia kuziba mapengo ya ugharimiaji wa miundombinu yake, ili kuwezesha malengo ya maendeleo endelevu iliyo nayo.

Hapo inajulikana kwamba vyanzo vikuu vya mapato ya serikali duniani huwa ni kodi, sambamba na vyanzo kama misaada kwa baadhi ya serikali zenye uwezo wa chini.

Penye shida mbalimbali za mahitaji tajwa, ni bahati mbaya lingine hujitokeza kwamba hakuna mipango thabiti katika kupanga uwiano sahihi kati ya mahitaji na bajeti kiserikali na hilo hushuhudiwa sana katika ngazi ya serikali za mitaa.

Bajeti ya nchi hasa katika serikali za mitaa kuna mengi hujitokeza kuachwa nyuma mahitaji ya umma katika kukidhi vifaa vinavyohitajika kusimamia rasilimali za miundombinu katika kipindi chote cha mahitaji ya umma, iwe huduma za muda mfupi au za kudumu.

Katika mazingira ya utawala bora duniani kote, serikali za mitaa na serikali kuu, kila moja kwa nafasi yake inatakiwa kuimarisha usimamizi wa rasilimali za miundombinu pamoja na mwongozo wa namna ya kutumia zana hizo, katika mazingira ya changamoto ilizo nazo katika jamii, kiuchumi na kimazingira.

> **Hali ya kuzingatia umadhubuiti katika 'upya na uimara' wa rasilimali za zamani, mara nyingi kuna kusahaulika namna rasilimali mpya zinapojengwa, pale pasipo kuwekwa muundo wa usimamizi utakuwa wa uhakika, jumuishi na endelevu katika huduma muhimu, kunakuwepo kasoro.**

Hali ya kuzingatia umadhubuiti katika 'upya na uimara' wa rasilimali za zamani, mara nyingi kuna kusahaulika namna rasilimali mpya zinapojengwa, pale pasipo kuwekwa muundo wa usimamizi utakuwa wa uhakika, jumuishi na endelevu katika huduma muhimu, kunakuwepo kasoro. Nikirejea pale yalipo makazi yangu eneo la Mwenge - Mlalakuwa, wilaya ya Kinondoni jijini, Dar es Salaam, nashuhudia namna wazazi wanapata changamoto ya kupasuka kwa mifumo ya majitaka kwa muda mrefu na hapo kuna sababu kuu kwamba huo ni mfumo mkongwe, aina ya mazingira yanayokumbusha haja ya kuboreshwa mfumo wa majitaka kuwanusuru wakazi katika mazingira endelevu kwao.

Daima panapokosekana suala la utunzaji miundombinu, kunatakiwa kujiweka katika mazingira magumu. Kuna wakati nadodosa takwimu za nchi nyinginezo na kubaini ni jambo linalogharimu wakati fulani hadi asilimia ya pato la ndani ya nchi, kuwekeza katika eneo la miundombinu ya mfumo wa maji safi na majitaka.

Pale penye miundombinu isiyotunzwa rasilimali zake, huwa kuna uwezekano mkubwa wa kushindwa kufanya kazi inavyopaswa, hata kukatisha huduma stahiki kwa umma na nyinginezo, ikiwamo kama usafiri, kupatikana majisafi na majitaka au usimamizi wa taka ngumu.

Kuna maeneo tunawaza kutumia uzoefu wake kujifunza. Suala la uahatarishi wake katika mazingira magumu kama penye mlipuko wa maradhi Uviko 19, ni suala muhimu sana kwa umma, ikiendana na madhara ya matatizo kama vile hali mbaya ya hewa au dharura za kiafya, mlipuko huwa na athari mara mbili zaidi.

Wakati serikali inaendelea kuboresha miundombinu katika eneo hilo, kuna njia muafaka ya kutatua changamoto za majitaka yanayosambaa mitaani katika maeneo wanayoishi watu na kuzalisha kero kubwa kwa umma jirani, hata kuhatarisha afya ya wakazi wa eneo na hasa watoto wanaocheza maeneo ya jirani na majitaka. Hili ndilo niseme linatusibu wakazi wa Mwenge - Mlalakuwa.

Nikiwa ni sehemu ya wakazi hao, nina upande wa pili wa shilingi, nikipongeza juhudi za Rais Samia Suluhu Hassan, kujali umma kwa kuboresha huduma za miundombinu ya majitaka katika eneo hili.

Ili kuitikia wito wa Rais Samia, ni vyema wananchi kwa pamoja kuwa mstari wa mbele katika kushirikiana kuilinda miundombinu hiyo, ili iweze kudumu kwa muda mrefu na hivyo kuboresha maendeleo kwa ujumla wake.

Matokeo yake serikali kuu na serikali za mitaa zinapaswa kutafuta rasilimali muhimu kama vile rasilimali za miundombinu ya umma, kwani ni msingi wa uchumi wa taifa na kushughulikia athari za kiuchumi na kijamii.

TANGAZO

MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

Ina Ithibati ya ISO 9001:2015

# TAARIFA KWA UMMA

## MABORESHO YA MTANDAO WA TRA

**Dar es Salaam, 08 Juni, 2022:**

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) inapenda kuwataarifu wadau wake na Umma kwa ujumla kwamba, tutafanya maboresho ya mtandao siku ya **Jumapili** tarehe **12.06.2022** kuanzia **saa 6:00 usiku** hadi **saa 12:00 asubuhi.**

Maboresho hayo yataathiri upatikanaji wa mifumo yote ya TRA kama vile Tovuti ya **TRA, TANCIS, e-filing, EFDMS, TIN, Mfumo wa Malipo (RGS)** kwa watumiaji wote, Hivyo Huduma zote za mtandao hazitapatikana katika kipindi chote cha maboresho.

Baada ya maboresho hayo, maunganisho binafsi ya kimtandao baina ya TRA na wadau wake yanaweza kuathirika pia. Hivyo hali hii ikijitokeza, tafadhali wasiliana na dawati letu la huduma kwa namba **+255 786 899 900** kwa msaada na utatuzi wa tatizo lililojitokeza.

TRA inaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza kupitia maboresho hayo kwani tunatarajia yataboresha huduma tunazozitoa.
Kwa taarifa zaidi, tafadhali wasiliana nasi kupitia WhatsApp namba **+255 744 233333** au tupigie simu namba **0800 75 00 75** au **0800 78 00 78** au **0800 11 00 16**, Barua pepe: **huduma@tra.go.tz**. au **service@tra.go.tz**

***"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"***

Imetolewa na;
**MKURUGENZI WA HUDUMA NA ELIMU KWA MLIPAKODI**

216893902

# Biashara ya ukahaba yawakera madiwani

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MADIWANI wa Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha wameliagiza Jeshi la Polisi kuchukua hatua kwa watu wanaojihusisha na vitendo vya ukahaba ambavyo vinahatarisha mmomonyoko wa maadili kwa vijana wa wilaya hiyo.

Akizungumza kwenye kikao cha Baraza la Madiwani Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Erasto Makala, alisema biashara hiyo inavunja utu wa Mtanzania, hivyo hatua za kisheria zinatakiwa kuchukuliwa mapema kabla haijashamiri.

"Kupitia kikao cha baraza hili tunaagiza hatua kali za kisheria zichukuliwe kwa wale wanaojihusisha na biashara hii, maeneo yanayotajwa kwenye wilaya yetu wahusika wadhibitiwe kwani inaenda kinyume na maadili yetu," alisema Makala.

Aidha, aliwataka wamiliki wa baa zinazodaiwa kuwa na watu wanaofanya biashara hiyo kuitwa na kuonywa, lakini elimu itolewe kwa vijana kuelezwa madhahara yake ikiwamo namna inavyochangia maambukizi ya Virusi Vya Ukimwi (VVU).

Diwani wa Viti Maalumu, Josephine Gunda, alisema wahusika wa biashara hiyo kwa sasa wamehamia vijijini ambako wanatawanyika katika maeneo mbalimbali.

"Kuna maeneo ya vilabu ambayo pia watu wanauza sigara, bangi, wapo wadada wanatumika kwa huduma za haraka wanaenda kutuharibia watoto na mmomonyoko wa maadili kwa vijana wetu, unaenda kutokea endapo hatua hazitachukuliwa mapema.

"Mchana wamelala kuanzia saa 12 jioni wanaanza biashara hiyo. Makubaliano yanafanyika hadharani wakati watoto wetu wanakuwa bado wanaenda dukani hii ni hatari sheria zinapaswa kuchukuliwa haraka," alisema.

Madiwani wengine walichangia hoja hiyo kwa kusema kuwa endapo udhibiti hautafanyika mapema biashara hiyo itasababishia vijana wengi kuharibikiwa kimaadili.

Kupitia baraza hilo, wazazi wamekumbushwa kutumia muda kukaa na watoto wao kwa kuwafundisha masuala ya makuzi na kuwaeleza kuhusiana na mambo ambayo hayana afya kwenye jamii, namna ya kuyaepuka, lakini madhara yake endapo watajiingiza huko.




Ofisa Masoko wa Diamond Trust Bank Tanzania Ltd (DTB), Dennis Rauya (aliyesimama), akitoa mafunzo wakati wa kongamano iliyowaleta pamoja mawakala wote wa benki hiyo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Maabara ya kisasa SUA kugharimu mabilioni

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

SERIKALI imetoa Sh. bilioni 11.7 kwa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo, (SUA) kwa ajili ya ujenzi wa maabara ya kisasa na madarasa ya kufundishia na kujifunzia ili kuondokana na tatizo lililokuwa likikikabili chuo hicho.

Jengo hilo litakuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 3,205 kwa wakati mmoja, huku likijumuisha madarasa nane, maabara nane, ofisi saba, vyumba 11 vya maandalizi na stoo saba kwa ajili ya kuhifadhia vifaa na kemikali.

Makamu Mkuu wa SUA, Profesa Raphael Chibunda, alisema hayo wakati wa akitoa taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya chuo hicho katika kipindi cha kwanza cha uongozi wake wa miaka mitano.

Profesa Chibuda ameteuliwa tena kushika nafasi hiyo katika kipindi kingine cha miaka mitano na Mkuu wa Chuo Kikuu hicho Waziri Mkuu Mstaafu, Jaji Joseph Warioba.

Profesa Chibunda, alisema maabara zinazojengwa ni sayansi ya mimea, kupima ubora na usalama wa chakula, sayansi ya vina saba, darubini, maabara ya zoolojia, kompyuta, maabara ya maikrobaiolojia na maabara ya baiokemia.

Alisema mradi huo ulianza kutekelezwa Julai 2018 na unatarajiwa kukamilika Juni 2022 na maabara hizo ni za kwanza kwa ubora na ukubwa katika nchi za ukanda wa Afrika Mashariki na Kati.

Wakati huo huo, Prof. Chibunda, alisema SUA imekamilisha ujenzi wa maabara ya kisasa ya sayansi katika Kampasi ya Solomon Mahlangu iliyoko eneo la Mazimbu mjini Morogoro, ili kumaliza upungufu wa tatizo hilo.

Mradi huo umefadhiliwa na Serikali ya Kifalme ya Norway kupitia mradi wa Enhancing Pro - Poor Innovation in Natural Resources and Agricultural Value Chains (EPINAV) na tayari wanafunzi wameshaanza kusoma.

Prof. Chibunda, alisema mradi huo umetekelezwa kwa gharama ya Sh. bilioni 2.6 na tayari maabara hiyo inatumika pamoja na kupokea sampuli za kufanyiwa uchunguzi kutoka ndani na nje ya nchi.

Alisema jengo hilo lina maabara nne za sayansi, kemia na bailojia zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 100 kwa kila moja na vyumba vinne vya maandalizi ya masomo.

Mkuu wa Chuo cha SUA, Jaji mstaafu Joseph Warioba, alishukuru serikali na wadau wa maendeleo kwa kutoa fedha hizo za ujenzi wa miradi hiyo mikubwa ambayo imeweza kusaidia kutatua tatizo lililokuwa likikikabili chuo hicho.

Jaji Warioba aliahidi kusimamia kwa karibu SUA ili iweze kuendelea kutoa elimu bora hapa nchini.

## Mollel mgeni rasmi kongamano la kisayansi HKMU

**Na Joseph Mwendapole**

CHUO Kikuu cha Kumbukumbu ya Hubert Kairuki (HKMU), kimeandaa kongamano la kisayansi kwa ajili ya kujadili magonjwa ya mlipuko na kuweka mifumo imara ya afya.

Mgeni rasmi katika kongamano hilo linalotarajiwa kuanza leo jijini Dar es Salaam ni Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam na Makamu Mkuu wa chuo hicho, Profesa Yohana Mashalla, wakati akizungumza na Nipashe kuhusu kongamano hilo la siku mbili.

Alisema HKMU imekuwa ikiandaa kongamano kama hilo kila mwaka na kualika wanataaluma wengine kutoka vyuo vya elimu ya juu na taasisi zinazofanya utafiti.

Alisema kupitia makongamano kama hayo HKMU imekuwa ikitoa taarifa kuhusu tafiti ambazo wamezifanya ili ziweze kusaidia kutatua matatizo mbalimbali.

Alisema madhumuni ya kufanya hivyo ni kutoa elimu kwa umma kuhusu matatizo ya kiafya na mikakati wanayoifanya katika kutafuta majawabu ya matatizo ya kiafya.

"Kongamano letu ambalo ni la sita mwaka huu litafanyika Juni 10 hadi 11 na maudhui ya kongamano letu ni 'Kuimarisha huduma za afya katika kukabiliana na changamoto zinazojitokeza.'

Alisema walichagua maudhui hayo kutokana na tatizo lililojitokeza la UVIKO-19 ambao ulianzia China na kusambaa dunia nzima kwa muda mrefu.

Alisema mlipuko wa aina hiyo siyo wa kwanza wala wa mwisho kwani ipo iliyopita na itakayokuja, hivyo watafiti wanaona kwamba milipuko ya aina hiyo inaweza kutokea siku za baadaye.

"Kutokana na hali hiyo wanasayansi lazima tujiulize je, mifumo ya afya ya nchi yetu iko imara kiasi gani kukabiliana milipuko ya aina hii iwapo itajitokeza," alisema Profesa.

Alisema kama nchi haiko tayari basi kongamano hilo litasema mapungufu yaliyoko na je, nchi ifanye nini kuwa na mfumo wa afya ambao unaweza kuwa na nguvu na imara kukabiliana na milipuko kama hiyo inapojitokeza.

Prof. Mashalla alisema kongamano hilo litawashirikisha madaktari, wauguzi, watafiti, wanafunzi, walimu, NGOs na maprofesa na wawakilishi wa Shirika la Afya Duniani (WHO).

Alitaja washiriki wengine wanaotarajiwa kwenye kongamano hilo kuwa ni Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), (KCMC), Chuo cha Sayansi ya Afya Muhimbili (MUHAS).

# RC aagiza mmiliki salfa feki korosho ajisalimishe

**Na Abdallah Bakari,** MTWARA

MKUU wa Mkoa wa Mtwara, Brigedia Jenerali Marco Gaguti, ametoa saa 48 kwa mmiliki wa kiuatilifu cha salfa ya unga chapa Makonde kujisalimisha kwa mamlaka ya serikali mkoani humo kwa madai ya kusambaza kwa wakulima kiuatilifu feki.

Pia amesema tayari watu saba wanashikiliwa na Jeshi la Polisi mkoani humo kwa kukutwa na kiuatilifu hicho mifuko 2,100 katika wilaya za Tandahimba na Newala mkoani humo.

Alibainisha jana mjini hapa kuwa watu wanne ambao ni wafanyabiashara wamekamatwa katika Wilaya ya Newala wakiwa na mifuko 1,600 na wengine watatu katika wilaya ya Tandahimba wakiwa na mifuko 500 ya kiuatilifu hicho.

"Ninatoa saa 48 kwa mmiliki wa salfa chapa Makonde kujisalimisha katika mamlaka za serikali mkoani Mtwara ili atoe ushirikiano juu ya salfa hii...baada ya huo muda atatafutwa popote alipo na kukamatwa ili atoe ushirikiano," alisema Gaguti na kuongeza:

"Hawa tuliowakamata wapo katika taratibu za mwisho kuwafikisha mahakamani... na nitoe wito kwa wakulima kutotumia pembejeo nje ya zile zilizotolewa na serikali na watoe taarifa pindi wanapoona viuatilifu wasivyovifahamu," aliagiza.

Wakati huo Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM) Mkoa wa Mtwara umetoa wiki moja kwa mamlaka husika kuwachukulia hatua wale wote wanaohusika na usambazaji wa pembejeo hizo feki za korosho.

Mwenyekiti wa umoja huo Mkoa wa Mtwara, Naseeb Kanduru, alisema kuwa iwapo mamlaka husika zitashindwa kufanya hivyo, umoja huo utayaweka wazi majina ya wahusika wote wa kashifa hiyo ya pembejeo feki bila kujali wadhifa wala cheo.

"Mkuu wa Mkoa tunatambua kazi kubwa unayoifanya na uliahidi siku ile kuwa utafanya wewe mwenyewe, sasa kwa kuwa ilikuwa ahadi yako na hizo 'klipu' zipo, hawa wahusika tunakuomba ushughulike nao, taarifa ya mamlaka imethibitisha zipo hizo pembejeo tunataka tuone hatua zinazochukuliwa," alisema Kanduru.

Aliongeza kuwa wao kama umoja wa vijana watakaa kimya kwa muda mfupi baada ya hapo watawataja wote waliohusika bila kuhofia vyeo vyao.

Alifafanua kuwa umoja huo utahamasisha vijana wa mikoa mingine inayolima korosho kuhakikisha pembejeo zisizofaa kwa matumizi pindi zinakamatwa na kuteketezwa ili kunusuru anguko la uzalishaji wa zao hilo nchini.

"Tunapokuwa na viuatilifu ambavyo havina ubora, fatsiri yake ya kwanza nini, uzalishaji hautafikia malengo, tusipofikia malengo uzalishaji kile ambacho tulichowaahidi wananchi hakitafikia, lakini lazima tukubaliane, Rais alisema atatoa pembejeo bure kwa wakulima," alisema Kanduru.

Mwenyekiti huyo pia aliwashukia wabunge wa Mkoa wa Mtwara kwa ukimya wao katika sakata hilo la pembejeo feki huku wakulima wakiteseka.

"Kila mbunge anaongelea suala la maji, lakini kwenye hili wapo kimya, je, hawajui? Athari zinazoenda kuwakuta wananchi wao ambao wanaowaongoza, sasa mimi niseme tunazo taarifa za kutosha za mlolongo wa watu wote wanaohusika na tunajua wapo wakubwa wengine kwenye wilaya, mkoa hadi taifa ambao hawa watu wanawashikia," alifafanua Kanduru.

## DC ampa siku saba mwenyekiti wa kijiji

**Na Neema Hussein,** KATAVI

MKUU wa Wilaya ya Tanganyika, Onesmo Buswelu, ametoa siku saba kwa Mwenyekiti wa Kijiji cha Bulamata na kamati ya ujenzi kuhakikisha kituo cha afya Bulamata kinakamilika na kuanza kutoa huduma kwa wananchi.

Buswelu alitoa maagizo hayo wakati alipotembelea katika kituo hicho kwa ajili ya kukagua maendeleo ya ujenzi juzi na kubaini mradi huo kusuasua.

Alisema upo uzembe kuanzia kwa mwenyekiti wa kijiji, ofisa mtendaji wa kijiji na kata na mhandisi hafuatiliwi kikamilifu, hivyo akaagiza kuwekwa taa katika eneo hilo ili kazi ifanyike mchana na usiku.

"Rais ametoa fedha zifanye kazi sio zisimame, hayupo aliye mkubwa zaidi ya Rais, atoe fedha aagize kazi ifanyike anakuwapo mmoja anakwamisha halafu haji kwenye kazi, haipo hiyo," alisema Buswelu.

Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Bulamata alisema awali walipokea shilingi milioni 250 kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho ambapo walitegemea kuwe na majengo matatu likiwamo jengo la maabara.

Fundi mkuu wa mradi huo, Jailos Nyandwi, alisema mradi huo umechelewa kutokana na vikwazo mbalimbali ikiwamo ucheleweshwaji wa vifaa na malipo ambao unapelekea mafundi wengi kukimbia.

"Kuna baadhi ya matukio kama simenti hazikufika kwa wakati, tukiuliza kamati wanadai kwamba usafiri, lakini kamati ya ujenzi wilaya inatufanya tusiende kwa kasi zaidi maana kila hatua inatakiwa tuwasiliane nao waje kukagua lakini hawafiki kwa wakati," alisema Nyandwi.

Imeelezwa kuwa kituo cha afya Bulamata kilitakiwa kikamilike Mei 23 mwaka huu, lakini mpaka sasa hakijakamilika.




Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Balozi Dk. Batilda Burian, akizungumza na wageni waalikwa wakati wa hafla ya chakula cha jioni iliyoandaliwa na Benki ya Exim kwa ajili ya wateja wadogo na wakubwa wa mkoani humo hivi karibuni, ili kujadili fursa za biashara na kutambulisha huduma mpya za benki hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TANESCO yapata mwarobaini kudhibiti vishoka wa umeme

**Na Daniel Limbe,** CHATO

SHIRIKA la Umeme nchini (TANESCO) limedai kuja na mkakati madhubuti wa kudhibiti vishoka waliokuwa wakilipaka matope na kusababisha baadhi ya wateja kutoridhishwa na huduma zake.

Katika kukabiliana na vishoka hao, sasa wateja watalazimika kuomba huduma ya kuunganishiwa umeme kwa njia ya simu badala ya kuwatumia vishoka na wengine kutumia gharama kubwa kwenda ofisi za TANESCO.

Meneja wa TANESCO Wilaya ya Chato mkoani Geita, Emily Ntazimila, aliyasema hayo jana baada ya kumuunganishia huduma ya umeme, Getruda Mremwa, mkazi wa Kijiji cha Zanzibar, Kata ya Bwina wilayani hapa.

"Shirika letu limekuja na mpango kabambe wa kidijitali maarufu kwa Ni-Konekt ambao unamrahisishia mteja wetu kuomba huduma ya kuunganishiwa umeme kwa njia ya mtandao... njia hii inawasaidia wateja wetu kujiepusha na vishoka ambao awali walikuwa wakiwatapeli fedha zao," alisema Ntazimila.

Ofisa wa huduma kwa wateja wa shirika hilo wilayani hapa, Salma Mbwana, alisema hakuna haja kwa wateja wanaohitaji huduma ya umeme kutembea umbali mrefu kwenda ofisi za TANESCO badala yake watumie huduma ya Ni-Konekt ambayo inapatikana kwa kuandika namba *152*00# kupitia simu ya mkononi.

"Baada ya huduma ya Ni-Konekt kuzinduliwa rasmi juzi kwenye kanda yetu maombi ya wateja imekuwa kubwa ikilinganishwa na awali walipokuwa wakilazimika kufika kwenye ofisi zetu... hata hivyo njia hii ni mwarobaini kwa vishoka waliokuwa wakijipatia fedha kwa njia ya wizi kwa wateja wetu," alisema Mbwana.

Mbali na kuonyesha furaha yake, Getruda Mremwa, alipongeza huduma ya Ni-Konekt baada ya kuunganishiwa umeme nyumbani kwake ndani ya saa 24 baada ya kuomba kupitia mfumo huo juzi.

Alilitaka shirika hilo kuendelea kutoa elimu zaidi kwa wananchi ili watambue huduma mpya ambazo zimeanza kutolewa na TANESCO hasa kwa wananchi waliopo vijijini.

# 'Moshi mweupe' ujenzi wa kiwanda cha mbolea

SERIKALI imeliarifu Bunge kuwa kuna wawekezaji wamejitokeza kuwekeza katika viwanda vya kuzalisha mbolea kwa kutumia gesi asilia.

Naibu Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Exaud Kigahe, alibainisha hayo jana bungeni alipojibu swali la nyongeza la Mbunge wa Kilwa Kusini (CCM), Ally Kassinge.

Mbunge huyo alitaka kujua serikali imefikia hatua gani kwenye mazungumzo yake na mwekezaji wa ujenzi wa kiwanda cha mbolea Kilwa Masoko kwa kutumia malighafi ya gesi asilia.

"Kwa muda mrefu serikali kupitia TPDC imekuwa na mazungumzo ya ujenzi wa kiwanda cha mbolea Kilwa Masoko kitakachotokana na malighafi ya gesi asilia na mara ya mwisho tumepewa taarifa kwamba serikali ipo kwenye mazungumzo na mwekezaji. Je, mazungumzo kati ya serikali na mwekezaji yamefikia hatua gani?" alihoji.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Kigahe alisema mipango ya serikali ni kuhakikisha gesi asilia iliyopo mkoani Mtwara inatumika kuzalisha mbolea ambapo Shirika la Maendeleo ya Petroli (TPDC) limetenga eneo hilo na kuna wawekezaji wamejitokeza kufanya uwekezaji huo.

Alisema azma ya serikali ni kujitosheleza kwenye uzalishaji wa mbolea nchini ambapo mahitaji ya sasa ni tani 700,000 na uzalishaji ulipo sasa si zaidi ya tani 100,000.

"Serikali inafuatilia sana jambo hili kuhakikisha majadiliano hayo yanakamilika mapema, tunafanya majadiliano ya kuona namna gani tutawavutia ili kuweza kutumia gesi hiyo ikiwamo bei," alisema.

Katika swali la nyongeza, Mbunge wa Nachingwea (CCM), Amandus Chinguile, alitaka kujua mkakati wa serikali wa kufufua viwanda viwili vya kupangua korosho na cha kuzalisha mafuta.

Akijibu swali hilo, Kihage alisema serikali ilifanya ubinafsishaji wa viwanda 156 na tathmini iliyofanywa mwaka 2017 ilibaini viwanda 88 vilikuwa vinafanyakazi na viwanda 68 vilikuwa havifanyikazi vizuri.

Alisema serikali imefanyia kazi ya kuvirudisha viwanda 20 vikiwamo vya kuzalisha mafuta na kubangua korosho vya Nachingwea.

Alisema kuna viwanda wameviweka kwenye eneo huru la uwekezaji na serikali inatafuta uwekezaji ili viwanda vivyo viweze kuzalisha mafuta na kubangua korosho kwa ajili ya mauzo ya nje.

Katika swali la msingi, Mbunge wa Kawe (CCM), Askofu Josephat Gwajima, alihoji mkakati wa serikali kusaidia wenye viwanda vilivyokufa au havifanyi kazi kwa sababu mbalimbali ikiwamo kiwanda cha kutengeneza mafuta ya kupikia kilichoko Salasala jimboni kwake.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Kihage alisema mkakati wa serikali kupitia utekelezaji wa Blue Print ni kuhakikisha vikwazo vyote vilivyokuwa zinavikabili viwanda hivyo vinatatuliwa ili viwanda hivyo vifanye kazi ikiwamo kiwanda cha mafuta ya kupikia cha Famili.



Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia wenye Ulemavu, Ummy Nderiananga (kushoto), akizungumza na wawakilishi wa viongozi wa Jumuiya ya wenye Ualbino, Joseph Magutu (kulia) na Selina Banzi, walipokutana kwenye viwanja vya Bunge, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Serikali yateta na WB ujenzi daraja Jangwani

SERIKALI imesema inaendelea na mazungumzo na Benki ya Dunia (WB) ili kupata fedha kwa ajili ya ujenzi wa daraja jipya la Jangwani jijini Dar es Salaam.

Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Godfrey Kasekenya, alibainisha hayo bungeni jijini hapa jana alipojibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Asha Abdullah Juma.

Mbunge huyo alihoji lini serikali itajenga daraja katika eneo la Jangwani, Barabara ya Morogoro jijini Dar es Salaam ili kuondoa usumbufu na adha wanazopata wananchi hasa wakati wa mvua.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Kasekenya alisema kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi wa daraja jipya la Jangwani chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia ili kutatua tatizo la mafuriko imekamilika.

Alisema serikali inaendelea na mazungumzo na Benki ya Dunia ili kupata fedha kwa ajili ya ujenzi.

Katika maswali yake ya nyongeza, mbunge huyo alisema kwa kuwa mvua itaendelea kunyesha na tope, taka, magugu na mafuriko nayo yataendelea kuwapo, hivyo akahoji mpango wa dharura wa serikali wakati ikisubiri mpango huo mkubwa wa ujenzi wa daraja ambao unaonekana utachukua muda mrefu.

"Hapo siku za nyuma serikali ilieleza mpango mzuri wa kuendeleza eneo lile ili kuondokana na changamoto eneo lile la Jangwani ikiwamo kuunganisha pembezoni hadi daraja la Selander, ninaomba kuuliza serikali ule mpango mzuri umeishia wapi?" alihoji.

Akijibu maswali hayo, Kasekenya alisema kuna mpango wa dharura ambao unatumika kuhakikisha daraja hilo linapitika licha ya mvua kuendelea kunyesha.

"Tumemuweka mkandarasi maalum wa lile daraja ambaye kila baada ya mvua kunyesha anaondoa mchanga, udongo na taka ngumu mita 500 juu na mita 500 chini ili kuruhusu maji yapite na changamoto hii inasababishwa na watu kufanya kazi karibu na mto.

"Nitoe rai wanaofanya kazi karibu na mto wasisogee karibu na kingo za mto ambazo zinasababisha kushindwa kupita kwa maji darajani," alisema.

Hata hivyo, alisema mpango wa kuendeleza bonde la Jangwani upo kupitia DMDP na pia serikali imeamua itajenga daraja la juu (Flyover) katika barabara inayounganisha makutano ya Fire na Magomeni.

# Halmashauri 24 zasajili vikundi PPRA kisheria

OFISI ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) imesema mpaka kufikia mwezi Mei mwaka huu, halmashauri 24 kati ya 184 zimekwishavitambua na kuwezesha usajili vikundi 88 katika Mamlaka ya Kudhibiti Ununuzi wa Umma (PPRA) ikiwa ni kigezo cha lazima cha kisheria cha kuwezesha kundi la wanawake kupata zabuni za ununuzi.

Naibu Waziri wa Ofisi hiyo, Dk. Festo Dugange, aliyasema hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Anastazia Wambura.

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji uzingatiaji wa Sheria ya Ununuzi inayozitaka halmashauri kuhakikisha asilimia 30 ya fedha za ununuzi zinakwenda kwenye kampuni za wanawake.

Dk. Dugange akijibu swali hilo, alisema Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2011 inaelekeza taasisi nunuzi zote kutenga asilimia 30 ya bajeti inayotengwa katika ununuzi kwa ajili ya makundi maalum ambayo ni makundi ya vijana, wanawake, wazee na watu wenye ulemavu.

"Serikali inaendelea kuzielekeza halmashauri zote nchini kuhamasisha vikundi kujisajili na kutenga kiwango cha asilimia 30 ya bajeti ya ununuzi kwa vikundi hivyo vikiwamo vikundi vya wanawake," alisema.

Katika maswali yake ya nyongeza, mbunge huyo alisema kasi ni ndogo ya utekelezaji wa sheria hiyo na kuhoji mpango wa serikali kuondoa vikwazo vilivyoko kwenye utekelezaji wa sheria hiyo.

Naibu Waziri Dugange alikiri kuwa kasi bado ni ndogo na serikali imeweka utaratibu wa kuhamasisha vikundi kunufaika na hiyo asilimia 30 kwa kupitia Maofisa Maendeleo ya Jamii na kutoa elimu kujisajili PPRA.

Aliwaelekeza wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini kuhakikisha kigezo hicho kinazingatiwa kwenye bajeti kwa kutenga asilimia 30 ya ununuzi huo na kuhamasisha vikundi hivyo kujisajili PPRA.




Habari zote: Augusta Njoji , DODOMA




Wabunge wanapokuwa waajiri wa mawaziri




BUFE

IJUMAA JUNI 10, 2022

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

## MLEZI PEKEE BIBI YAO KIKONGWE...

# Yatima wenye njaa, nyumba nusura kubomoka, hadi Diwani kuwaopoa

**Na Julieth Mkireri, KIBAHA**

“NDOTO yangu ya kufikia malengo yangu ilizimwa baada ya kujikita zaidi kuhudumia ndugu zangu na kukosa muda wa kujisomea ninapokuwa nyumbani,” ndivyo anaeleza Mohamed Hamis.

Mohamed ni kijana anayeishi Mtaa wa Bamba, katika kata ya Kongowe, iliyoko katika Halmashauri ya Kibaha Mjini, ambaye katika familia yao walizaliwa watano, akiwa na simulzi ya safari ngumu ya maisha.

Anaeleza kuwa wazazi wake walifariki akiwa anasoma darasa la tano na kuwaacha chini ya uangalizi wa bibi yao Mwasiti Said, ambaye hakuwa na uwezo wa kufanya kazi inayowapatia chakula, wala mavazi.

Mohamed anasimulia kwamba kaanza kujihami kimaisha, kwa kufanya kibarua cha kuuza kuku kwenye banda la mtu, ili anapopata fedha zimsaidie yeye na ndugu zake wanne pamoja na bibi yao.

“Nilimaliza darasa la saba nikaendelea na shule ya sekondari, lakini kutokana na hali ngumu ya maisha yetu, niliendelea kutumia muda wa jioni kuendelea na kibarua changu ili wadogo zangu wapate chakula na fedha ya kwenda nayo shule,” anasema.

Anasema kutokana na kukosa muda wa kujisomea, hakufaulu mtihani wake wa kuhitimu elimu ya sekondari na hivyo ndoto zake za kuendelea mbele kukwama rasmi, hapo akihamia aliko sasa. Akajikita katika kufanya vibarua kwenye shughuli za kilimo, pia wakati mwingine



Familia ya Bibi Mwansiti Saidi, katika picha ya pamoja na Diwani Lydia Mgaya (kushoto) katika makazi yao mapya ya muda. **PICHA: JULIETH MKIRERI.**

amekuwa akisaidia mafundi kwenye shughuli za ujenzi kupata fedha za kujikimu na familia yao.

Mohamed anasema, mbali ya kuwa na ugumu wa kupata chakula, pia nyumba waliyokuwa wanaishi ilikuwa ni katika hali mbaya, ikiruhusu maji kuwafikia pale mvua zinaponyesha, kwani upande mmoja ulinama ukiwa katika hatua za kuanguka muda wowote, jambo ambalo lilikuwa linatishia hata usalama wa maisha yao.

“Wakati tukipitia haya yote kwenye maisha yetu hakuna ndugu aliyeguswa kutusaidia, tulikua tukihangaika wenyewe na dada yangu aliyekuwa anasoma sekondari kutokana na hali zetu aliingia kwenye vishawishi kukatisha masomo kwa kupata mimba,” anasimulia, akisema dada huyo sasa anajishughulisha na biashara ya kuuza chakula, ili kusaidia huduma mbalimbali kwenye familia yao.

Anasema wakiwa wanapitia maisha hayo magumu na bibi yao ambaye amekuwa mwangalizi wa familia, ndio alitokea Diwani wa Viti Maalumu Kibaha Mjini, Lydia Mgaya, aliguswa na uhalisia huo na kuwa ahidi kuwajengea nyumba, kazi anayoitekeleza.

Anaeleza, walitolewa katika nyumba hiyo na Diwani Lydia, ili aanze kuwajengea nyumba ya kudumu na kwa sasa wanaishi katika nyumba ambayo ni yenye mazingira bora, wakisubiri nyumba wanayojengewa ikamilike wahamie huko.

Akizungumza kuhusiana na hali ya maisha na wajukuu wake watano. Bibi Mwansiti Said, anasema mazingira waliyokuwa wakiishi awali kabla ya nyumba yao kubomolewa, yalikuwa hatarishi kwani nyumba ilikuwa inaelekea kuanguka.

Mwansiti anaeleza kuwa tangu watoto hao walipofiwa na wazazi wao, ameendelea kuishi nao pamoja na kuwa katika hali duni, lakini kwa kuwa hakukuwa na ndugu mwingine wa kusaidia, ameendelea kubaki nao hadi sasa..

Anamshukuru Diwani Lydia, kwa hatua ya kuwajengea nyumba ya kudumu ambayo ikikamilika itakuwa msaada kwao na kuishi katika mazingira mazuri na bibi huyo anaomba wahisani kujitokeza kumuunga mkono Lydia, ili kukamilisha ujenzi huo waweze kuhamia na kuondoka katika mazingira wanayoishi sasa ambayo si salama.

Diwani Lydia anafafanua hapo akisema, aliguswa kuanza kuwajengea nyumba watoto hao yatima baada ya kushuhudia ubovu wa nyumba wanayoishi. Anaeleza:”Nilifuatwa na baadhi ya wanawake wa Kongowe ambao waliniona nikiwa nasaidiana na wazee kukandika nyumba zao za udongo ambazo zilikuwa mbovu”

Anasema alifika katika nyumba hiyo na kujionea hali yake na kujadiliana na watoto hao na bibi yao kubomoa na wao waweze kuhamia sehemu nyingine, ili kutafuta miti na kujenga upya.

Lydia anasema kwa saaa nyumba hiyo iko katika hatua ya umaliziaji ambayo imesimama kwa muda kutokana na kukosa fedha, ikihitaji kiasi cha Sh. Milioni saba kwa ajili ya kununua vifaa vilivyosalia kumalizia ujenzi na kuiruhusu familia hiyo ya watoto yatima kuhamia.

Mmoja wa majirani wa familia hiyo, Amir Rashid anaeleza kuwa familia hiyo kabla ya nyumba yao ya awali kuvunjwa walikuwa wakiishi katika mazingira hatarishi, anasema nyumba hiyo ya awali ilichakaa na ilikuwa inakaribia kudondoka, hivyo kitendo alichofanya Diwani huyo ni kuokoa watoto wao wasiangukiwe na kukosa mahala pa kuishi.

Rashid amempongeza Lydia kwa uamuzi wake wa kuijengea familia hiyo nyumba huku akiomba wadau kumuunga mkono kumalizia ujenzi na watoto hao waweze kuhamia.

UCHUMI

MPAKA KIELEWEKE BAADA YA KUPEWA JUKUMU ...

# Wataalamu TARI Ilonga wanavyokesha kwenye operesheni kupatikana mbegu bora mafuta alizeti

- Wameibua aina mbili, 'kazi kwao' wakulima
- Waunda Vituo Mbegu Kanda kufuta urasimu
- Kupewa darasa, Kusambaziwa waliko shamba

**Na Renatha Msungu, aliyekuwa KILOSA**

WIKI hii kumeshuhudiwa tamko la serikali bungeni kuanza operesheni ya kufungua milango ya uwekezaji mkubwa kitaifa katika uzalishaji sukari na mafuta ya kula, wawekezaji wakitangazwa Sh. bilioni 78 zinaingia benki wakope, ili kuwekeza kwenye mazao hayo.

Inapoangaliwa katika suala la mafuta ya kula, mbali na wawekezaji wa mradi, mwenyeji na mratibu wake mkuu ni Taasisi ya Utafiti wa Mbegu nchini (TARI), ambayo tangu mapema imeshabainisha mikakati yake ya kuiwezesha serikali kudhibiti tatizo la uhaba wa mafuta.



Mkurugenzi wa Taasisi ya Utafiti wa Mbegu nchini (TARI) Dk, Mkamilo,akiwa na Mkurugenzi wa TARI Ilonga Dk. Lameck Makoye (aliyesimama kati),katika shamba la alizeti. Kushoto ni Mratibu wa Alizeti nchini,Frank Reuben.

Nipashe imefuatilia kwa kina mkakati huo ilioupanga kuhakikisha uzalishaji mafuta ya kula kitaifa unachukua nafasi yake, hususani zao la alizeti, kwa kuzalisha mbegu bora zinazotoa mafuta kwa wingi na zinapatikana ifikapo msimu wa kupanda zao hilo shambani.

Mbegu hizo aina zake zinatajwa kwa majina 'TARI-ILO' na 'TARI-NA' zilizofanyiwa utafiti na Kituo cha Utafiti wa Kilimo -TARI Ilonga, ambacho kinasambaza mbegu sahihi, pia kuwapatia elimu sahihi wakulima namna sahihi ya kuzihudumia, kuanzia maandalizi, kupanda hadi mavuno.

Ni elimu inayotolewa katika mashamba darasa maalum ya wakulima, ikisimamiwa na maofisa ugani kwa kushirikiana na watafiti wa TARI Ilonga, ili kilimo bora ikiwemo alizeti, kiwe chenye manufaa kwa wakulima na taifa kwa ujumla.

**WATAALAMU MBEGU**

Mratibu wa Mbegu Kitaifa, Frank Reuben, anasema ni mbegu zenye uwezo wa kukinzana na wadudu waharibifu wa alizeti pindi wanatokea shambani, hata kuwezesha kumlinda mkulima

"Mbegu hizo pia zinastawi sana katika mazingira ya nchi yetu, hivyo wakulima wanapaswa kuzichangamkia kwa sababu zitawapa mavuno mengi, ikiwemo mafuta," anafafanua.

Anataja mikakati waliyojiwekea inajumuisha kuanzishwa vituo vya utafiti wa mbegu katika kanda, kurahisisha kuwahudumia wakulima kupata mbegu aina tofauti, wakishirikiana na taasisi wazalishaji kama vile Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Magereza na World Vision, wakiongeza mashamba darasa kuotesha mbegu hizo.

Reuben anaeleza haja ya kuhakikisha tatizo la mafuta linapungua nchini, kama sio kumalizika, huku TARI imeshatafiti kwa kina kujua wanachohitaji wakulima ili waweze kuzalisha mafuta kwa wingi, kupitia zao la alizeti katika maeneo mbalimbali nchini.

Anaeleza, katika utafiti wao uliolenga zaidi mipango na sera za nchi zinazohitaji kupunguza uhaba wa mafuta hasa ikizingatiwa ongezeko la hitaji ya mafuta ya kula kila mwaka,watafiti waligundua aina mbili za mbegu bora zinazokabili wadudu waharibifu wa zao hilo.

Mratibu anafafanua zaidi, kuwa baada ya majaribio ya mbegu hizo katika mashamba darasa ya wakulima chini ya usimamizi wa wataalamu wa kilimo ambao wamekuwa wakitoa elimu kwa wakulima, matokeo chanya kwa wakulima yameshuhudiwa.

"Mbegu hizi ni bora sana, kwa sababu zina faida kubwa ya kukinzana na wadudu waharibifu, pia zinatoa mafuta mengi pindi zikivunwa na baadae kukamuliwa mafuta," anasema .

Mtaalamu huyo ana ufafanuzi kwamba TARI Ilonga sasa ina jukumu la kuzalisha kwa wingi mbegu hizo katika vituo vyao vya kanda, kuhakikisha zinawafikia wakulima katika mikoa yote inayohitaji kuzitumia katika msimu ujao wa kilimo cha alizeti.

**USAMBAZAJI ULIVYO**

Usambazaji wake, anasema ni kupitia vituo kanda walivyovianzisha, akivitaja kuwa ni za kanda: Ziwa, Kaskazini, Nyanda za Juu Kusini, Kati pamoja na Mashariki, kote kukiwapo vituo vya utafiti wa mbegu.

Mratibu huyo anafafanua kwamba hadi sasa alizeti inashika nafasi ya nne katika mazao yanayopewa kipaumbele, hivyo serikali inaipa msukumo hata kufikiwa mwitikio mkubwa kwa wakulima kitaifa kutaka kuzalisha alizeti.

"Mbegu hizi ni aina mbili zinazosambazwa kwa wakulima katika mikoa mbalimbali, zinakwenda kujibu malengo tuliyojiwekea, ili kupunguza uhaba wa mafuta," anasema Reuben, akiwa na ufafanuzi zaidi:

"Tumepanga kushirikiana na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT),Magereza na World Vision kuhakikisha wanazalisha mbegu bora za alizeti ambazo zitasambazwa kwa wananchi kwa ajili ya kuzitumia msimu ujao wa kilimo."

**USHIRIKI SEKTA BINAFSI**

Reuben anasema, tayari wanashirikiana na kampuni binafsi za kuzalisha mbegu nchini, lengo ni kupata mbegu bora za alizeti zitakazowasaidia wakulima kujikwamua kiuchumi, kwa kupata mazao mengi zaidi katika uwiano wa eneo lilelile, kulinganisha na ilivyokuwa awali wakipata kidogo.

Anafafanua, kuna jumla ya kampuni zaidi ya 20 za kilimo wanazozipa mbegu bora na kisha zinaenda kuwasambazia wakulima katika maeneo waliko, ili kuhakikisha wanakuwa katika kilimo chenye tija kwa manufaa yao na taifa.

Reuben anaeleza kwamba kampuni binafsi na TARI zimeingia mkataba na baadhi ya kampuni, zitakazopewa ufadhili wa kuzalisha mbegu kwa kushirikiana na wakulima kupitia kilimo cha mkataba, lengo kuongezauzalishaji na upatikanaji mbegu nchini.

"Ushirikiano huo unasaidia kujua mahitaji ya mbegu kwa wakulima kabla ya msimu kuanza, kwa sababu kampuni inawafuata wakulima kujua mahitaji yao," anaeleza Mratibu Reuben.

**FAIDA YA MBEGU**

Mratibu huyo wa Mbegu, anaeleza mtu anapopanda mbegu katika uwiano wa ekari moja, ana uwezo wa kuvuna kati ya kilo 800 ambayo ni wastani usiopungua gunia 12 au mpaka zaidi ikiwemo kupata mafuta mengi kulingana na uwezo wa utoaji mafuta iliyokuwa nao.

Anasema, wanachokifanya wao sasa ni kupanda mbegu hizo katika vituo vya kanda na msimu unapokaribia, wakulima wanazipata mbegu huko kirahisi, tofauti na kuzifuata mbali

Katika hilo, Reuben anasistiza ni muhimu kwa wakulima kuhakikisha wanalima kulingana na msimu ulivyo, wakiweka kando mazoea, jambo linaloowainua kiuchumi badala yake walime kwa tija ili kusonga mbele na kuwainua kiuchumi.

Baraka Daniei, Mratibu wa Uhaulishaji, Biashara na Mahusiano, anasema wao kwa nafasi yao wamekuwa wakikabili uelewa mdogo wa wakulima, wakiwafundisha hadu kufikia kiwango bora cha uelewa kwenye mabadiliko hayo ya mbegu na matumizi yake sahihi.

Mtafiti Daniel anaeleza maono yaliyoko ni kwamba, mbegu hizo zinaenda kuwainua kiuchumi wakulima kwa kufikisha bidhaa nyingi sokoni, kitaifa inamaliza tatizo la uhaba wa mafuta ya kula ndani ya miaka michache ijayo.

**MABOSI WA TARI**

Dk. Lameck Makoye, ndiye Mkurugenzi wa TARI Ilonga, anasema lengo la kituo hicho ni kufanikisha uzalishajiwa tani 80 za mbegu aina ya TARI-ILO na TARI-NA , zijitosheleze mahitaji katika msimu ujao wa kilimo cha alizeti kitaifa.

Anatoa mchanganuo wake kwamba, wamepanga tani 40 wazipeleke kwa wakala wa usambazaji mbegu nchini (ASA), ili kutengeneza mnyororo wa thamani wa alizeti, ASA wakisaidia kuzisambaza kwa wakulima.

Dk. Makoye anaeleza kwamba wamepanga kulima shamba la ekari 300 ya zao la alizeti msimu ujao, ili kukamilisha tani za mbegu aina hiyo walizoanga kuzisambaza kitaifa, baada ya mavuno.

Pia, anafafanua kwamba hadi sasa wanazidi kuboresha miundombinu ya maeneo yao kuhakikisha yanapata maji wakati wa kiangazi, kusaida kazi umwagiliaji mashamba hayo, pindi wanaotesha mbegu; TARI-ILO na TARI-NA.

Wito wake kwa wadau ni waangalie namna ya kuziwezesha taasisi mbalimbali katika utafiti, ili ziwe na miundombinu bora katika kusaidia kuongezeka uzalishaji wa mbegu bora zilizofanyiwa utafiti kumsaidia mkulima.

Mkurugenzi wa TARI Taifa, Dk. Geoffrey Mkamilo, anaeleza matarajio yao baada ya wakulima kuanza kutumia mbegu hizo, ni kutatuliwa tatizo la uhaba wa mafuta ya kula, kwa sharti wakulima hao watumie mbegu ipasavyo, ikiwemo kufuata ushauri wa watalamu wa kilimo na watafiti.

Dk. Mkamilo anaeleza wao TARI Taifa wameipa jukumu TARI Ilonga kutafiti uzalishaji wa mbegu za mazao mbalimbali, ikiwemo alizeti, jukumu wanaloendelea nalo kukidhi hitaji la taifa, kupatikana mafuta ya alizeti ya kutosha.

"Watafiti hawalali kila kukicha, wanafikiria kufanya utafiti ili kupata mbegu bora za alizeti zinazozalisha kwa wingi, ikiwemo zinazokinzana na wadudu waharibifu, zinazotoa mafuta kwa wingi," anasema Dk. Mkamilo, anayehitimisha kwa kuhimiza ushirikiano wa wakulima



Mratibu wa Zao la Alizeti nchini,Frank Reuben akionyesha zao hilo linavyotakiwa kustawi. **PICHA ZOTE: RENATHA MSUNGU.**

TAFAKURI YA MLALAHOI

# Wabunge wanapokuwa waajiri wa mawaziri






**NA JOSEPH KULANGWA**
Simu: +255 713 410008
barua pepe: jkulangwa@yahoo.com

FIKIRIA unafanya ziara kampuni ya kubwa ya kitajiri inayotikisa kwa mifano ya chaguo lako nchini, lakini kwa nyakati tofauti. Unaanzia kwa kampuni ya kwanza unakaribishwa, mara ghafla unamwona bosi mkuu na ndiyo tajiri mwenyewe yu kijana hivi, anapiga samasoti ofisini.

Unamwuliza, anakwambia watumishi wake wameshindwa kufanya kazi anayotaka ifanywe, hivyo analalamika kwa kupiga samasoti, ili wamwone na waifanye kazi hiyo.

Unatoka hapo,unakwenda tajiri wa pili naye anatikisa kitaifa, lakini umri wake tarehe zimesonga. Unamkuta analia huku amepiga magoti, naye unamwuliza, anakujibu kama wa kwanza, eti wafanyakazi wake wameshindwa kuzalisha bidhaa zake mbalimbali.

Bila shaka utashikwa na butwaa na kujiuliza hawa matajiri wa nchi hii wamekumbwa na nini? Kwa sababu, kwa hali ya kawaida ungekuta wafanyakazi wanapiga samasoti, sarakasi, magoti na kulia, kwa sababu wametimuliwa na waajiri.

Lakini, hayo yanafanyika tu katika Bunge letu, ambako waajiri wanawapigia magoti waajiriwa, ambako waajiriwa wanapiga samasoti, sarakasi na kuwalilia waajiriwa! Kwa kweli inatia mshangao!

Nimshukuru Spika, Dk Tulia Ackson, kwa kupiga marufuku tabia hii, ambayo ilitaka kuotesha matawi na mizizi katika mhimili huu unaoheshimiwa na Watanzania wote, kwa kuwasilisha matatizo yao na kuyapatia ufumbuzi.

Hata hili la kusema kuwa kulia ni hisia, lakini bado nalo naona linatakiwa kufanyiwa kazi, kwa sababu hata kwenye tamthilia tumeshuhudia watu wanalia au kujiliza, ili mradi ujumbe wa simulizi kusudiwa ufike.

Hivi ina maana wabunge bado hawajui kuwa ndio wawakilishi wa wananchi ambao ni waajiri wa mawaziri? Hawajatambua bado kwamba ndio wenye uwezo wa kuwafurusha mawaziri kwa kuwanyima mishahara yao?

Semina zote walizofanyiwa wakati wanaingia bungeni kwa mara ya kwanza, wakipewa makabrasha ya kanuni, taratibu na miongozo hakuna mahali waliambiwa kuwa ukitaka kumbana waziri basi shika shilingi.

Wanataka kutuambia kuwa kushika shilingi ya waziri si sawa na kuzuia mshahara wake? Kama walikuwa hawajui, basi na wajue kuwa kupiga samasoti, sarakasi, kupiga magoti na kulia hakuondoi shilingi kwenye mshahara wa waziri.

Wabunge wetu ni wawakilishi wetu sisi wananchi ambao tuna kura ya kumwingiza mbunge bungeni na akateuliwa kuwa waziri, hivyo tuna kura ya kumwondoa pale anaposhindwa kutimiza tuliyomtuma kufanya hapa.

Hivyo, suala la kujidhalilisha kwa kukwea meza na kuinua miguu juu huku umevalia suti, halina nafasi na ni vema kumsikiliza Dk. Tulia atulie.

Hivi mathalan mbunge yule mpiga samasoti angepitiliza au meza ikamteleza akatanguliza fuvu leo tungekuwa wapi? Tukiendekeza haya, kuna siku kweli yanaweza kuja mabaya zaidi.

Binafsi naamini Bunge halihitaji mihemko na hasira, bali utulivu, busara, mantiki, staha na umakini wa kusikiliza nini kinaulizwa, nani anauliza na nini kinajibiwa na nani anajibu.

Kuna nyakati huko nyuma, kulizuiwa Bunge mbashara, pengine kwa sababu hiyo hiyo ya kuzuia kiki zisizo na staha.

Wananchi waliokuwa na haki ya kufuatilia wawakilishi wao mbashara, waliikosa fursa hiyo.

Pia, ninyi waajiriwa wa wananchi, jaribuni kujitahidi kujibu maswali ya watu na kutoa maelezo ya ukweli jamani, msidhani huku tuliko hatufuatilii mambo yenu mnayosema. Si ajabu yapo ambayo tunakuwa hatujaridhika, lakini tunanyamaza tu.

Nimshukuru tena Spika Dk. Tulia kwa uamuzi wake. Jamani, watu hatulali tena mpaka kieleweke, mnapojibu jibu ni ya ukweli, mkitudanganya mjue tunaweka akiba kwa 2025.Ukibwagwa umebwagwa tu, mbeleko tena hakuna! Alamsiki!

BIASHARA

# Serikali yaamua kuwekeza mipango maendeleo ya vijana kupitia ubunifu

## • Maonyesho maalum yaja kitaifa
## • Asasi za UN rasmi kutoa 'sapoti'

**Na Maulid Mmbaga**

KUTOKANA na utandawazi na kasi ya ukuaji teknolojia, ubunifu ni nyenzo inayopaswa kupewa kipaumbele katika maendeleo ya sasa, ili kuruhusu mawazo mapya na mbadala yanayochochea mapinduzi ya teknolojia, biashara, kukua uchumi kitaifa na dunia.

Hadi sasa serikali imeshatoa kipaumbele kwa wabunifu, waanzilishi na wamiliki wa biashara, kuweka mikakati, ikiwamo kutunga sera itakayosaidia na kuwalinda, waweze kuendesha shughuli zao bila matatizo.

Mkurugenzi wa Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), Dk Amos Nungu, anaiambia Nipashe kwamba ubunifu umesaidia kutekelezwa mpango wa maendeleo kitaifa, hata kusaidia vijana wengi kujiajiri.

Anasema, wizara inayohusika na ufundi, sasa inaandaa mijadala kwa kuwashirikisha wabunifu na wadau wa biashara wakiwemo wa sekta binafsi, wanakusanya mawazo yatakayosaidia kuandaa sera kuwalinda katika kuendeleza ubunifu na biashara zao.

Anasema, waliandaa wiki ya ubunifu kwa mikoa 15, ikiwemo Dar es Salaam na imeshafanyika kwa kuendesha mijadala, midahalo na maonyesho ya ubunifu, mbalimbali kuwatangaza wabunifu.

"Wizara ya Elimu na Teknolojia imeamua tuwe na wiki ya ubunifu, kikubwa ni kwamba ubunifu tunaouongelea uweze kuwa ni ajenda ya kudumu na tunachokifurahia ni kupata mrejesho kutoka kwa wadau," anasema Nungu.

Anafafanua kwamba, serikali jukumu lake kuu ni kuweka mazingira wezeshi, ikiwemo sera, miongozo na miundombinu sambamba na kuandaa maonyesho, pia ikipokea maoni na kuyafanyia kazi.

Dk. Nungu anasema, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, ameshauri Wiki ya Ubunifu ifanyike kwa wilaya na mikoa yote na ndiyo maana mwaka, huu wameanza na mikoa 15, kwa matarajio mwakani watafanya nchi nzima.



Shughuli za ubunifu katika. **PICHA: MTANDAO.**

**TANTRADE NA VIPAUMBELE**

Mchumi kutoka Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TANTRADE), Deo Shayo, anasema sekta ya ubunifu na teknolojia, ni kati ya sehemu ambazo mamlaka hiyo imezipa kipaumbele kuendeleza biashara.

Anasema, wanajihusisha pia kufanya tathimini za ubunifu na kuzitafsiri kibiashara, kisha wanatoa ushauri, wakishirikiana na COSTECH kupitia programu yao ya kushindanisha wabunifu.

"Katika maonyesho ya Sabasaba na ya Export yaliyofanyika Dubai kwa zaidi ya miezi sita, kipaumbele kilitolewa katika ubunifu nchini kwenda kuzitangaza kule na kuwashawishi wawekezaji wakubwa kuwasaidia," anasema Shayo.

Anawashauri vijana kuwa watulivu na kujikita katika malengo, akifafanua anawashuhudia vijana wanajisahau kuanza kutumia fedha kununua vitu visivyokuwa na ulazima na wengine kuvurugana.

"Wengine wanaanza kama 'group' kundi na wakifikia 'level' hatua fulani unasikia huyu ameanza kutumia vibaya mali za kampuni na wengine kuwa na uoni hafifu," anaeleza.

Anatoa wito kwa serikali kuwapa vijana fursa na kuendeleza utamaduni wa pamoja, huku akisisitiza namna pekee ya kuwainua vijana ni kuweza kuangalia fursa mbele yao.

Mtaalamu wa Miradi kutoka Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), Emmanuel Nnko, anasema dunia sasa imebadilika, hivyo changamoto zilizopo haziwezi kutatuliwa kwa kutumia mbinu za zamani.

"Lengo letu ni kuweka jukwaa la wabunifu ili kuonesha bunifu zao zilizoleta utatuzi katika changamoto mbalimbali kwenye jamii," anasema.

Pia, Mwakilishi wa Mfuko wa Umoja wa Mataifa wa Maendeleo na Mitaji (UNCDF) Paul Damocha, anasema wanaunga mkono ubunifu kwa njia mbalimbali ikiwemo fedha za kuwasaidia kutengeneza mazingira wezeshi kwa wabunifu kujaribu ubunifu wao, kabla ya kupatiwa leseni.

Damocha anafafanua kwamba, watahakikisha wanaendelea kuwafadhili wabunifu kupata fedha na huduma za kitaalamu ili kuendeleza ubunifu walio nao.

Anasema, mfuko huo kwa kushirikiana na serikali wamekuwa wakitengeneza miongozo ya kuwasaidia wabunifu kuibua ubunifu unaotoa majibu ya matatizo yaliyopo katika jamii na kudhibiti kazi hizo ziweze kuwa na manufaa.

Mwanazuoni wa Masoko katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) Dk. Robert Suphiani, anasema chuo hicho kina zaidi ya wanafunzi 30,000 na kinatambua hakiwezi kuwapatia ajira wote kwa wakati mmoja, kwa sababu soko la ajira ni dogo.

Anasema: "Tumeadhimisha siku maalumu kwa ajili ya wajasiriamali wanafunzi ambao kuna walioanzisha na kufanya biashara mbalimbali na wabunifu.

"Hivyo, siku hiyo kila mtu alionyesha kitu alichofanya na kujenga uelewa zaidi wa vile ambavyo anaweza kufanya kwa siku za usoni.

"UDSM tuna utaratibu wa kuwakaribisha watu wenye mawazo mbalimbali, wajasiriamali wadogo wanapewa ofisi na vifaa vitakavyowasaidia katika hatua za awali, wanalelewa na wanapofikia kujiweza wanaenda kuendelea wenyewe."

Anaeleza kuwa chuo hicho pia kina mpango wa kuanzisha somo la ujasiriamali, ambalo kila mwanafunzi wa chuo atalazimika asome, bila ya kujali fani yake.

**TRA VS MAPUNGUFU**

Ofisa Msimamizi Mkuu wa Kodi, kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Stephan Kauzeni, anasema nafasi za ajira zimekuwa chache na watu wengi wamekuwa na utaratibu wa kubuni biashara zao, lakini wengi wakiogopa kodi wakiona ni tishio kwao.

Anafafanua kuwa TRA wanajipanga kuhakikisha wanawapa njia wabunifu, ikiwawezesha kujua watakavyoanza biashara, pia namna ya kulipa kodi

**INENAVYO BRELA**

Ofisa Sheria katika Ofisi ya Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) Vicensia Fuko, anasema lengo na mtazamo wao wanaipa biashara utu wa kisheria, kwa kuwasaidia wabunifu na wafanyabiashara kurasimisha biashara zao.

Anasema, watu wengi wako katika biashara zisizo rasmi, hivyo wamejipanga kuhakikisha wanawasaidia kufikia hatua kuwa zilizo rasmi wakizisajili.

"Ukiwa unabuni au una wazo lako bila kuwa na njia ya pili kuipa biashara utu wa kisheria, anaweza kufanya kazi ambayo haikuletei faida," anashauri Vicensia.

**MAONI YA TBS**

Ofisa wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS) Mathias Missanga, anasema kutambua mchango wa wabunifu katika maendeleo ya biashara na uchumi wa nchi, wamejipanga kuhakikisha wanawasaidia vijana wenye mwamko wa ujasiriamali kuzalisha na kusindika bidhaa zao kwa ubora, kuzingatia matakwa ya viwango.

Anasema wanawasaidia kujua namna bora ya usindikaji na viwango, ili bidhaa zao zinapoingia sokoni ziweze kushindana kwa kuvuka mipaka hasa kwenye soko la Jumuia ya Afrika Mashariki (SADC) nchi jirani zimeanza kuliangalia.

**WABUNIFU NA YAO**

Mbunifu, ambaye pia ni kiongozi katika Jukwaa la Wajasiriamali na Ubunifu (DUEF) kutoka UDSM, Ukende Mussa, anataja baadhi ya changamoto wanazokutana nazo katika ubunifu na biashara zao, ikiwemo kutojua pa kuuza bidhaa.

Wadau wengine wanasema pamoja na wabunifu kubuni mambo mbalimbali, lakini wamekuwa wakikosa msaada wa serikali na wakibaki na ubunifu ambao hauwanufaishi, hata nchi.

Pia, wanaishauri serikali kuangalia namna nzuri zaidi ya kuhakikisha bunifu ambazo zinagunduliwa zinakuwa na matokeo chanya, ikiwemo kuendelezwa na kutafutiwa masomo ya kukuza ubunifu huo.





## Wanafunzi vyuo vikuu wapewa jukumu sensa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia, Omary Kipanga, amewataka wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) kuhakikisha wanashiriki sensa ya watu na makazi, ikiwamo kutoa elimu kwa jamii ili kuisaidia serikali kupanga mipango ya maendeleo.

Sensa ya Watu na Makazi imepangwa kufanyika Agosti 23, mwaka huu, katika maeneo yote nchini.

Kipanga alisema hayo jijini Dodoma juzi wakati akifungua mdahalo wa kutathmini ushirikiano wa miaka 60 baina ya Serikali ya Tanzania na Marekani uliofanyika katika ukumbi wa UDOM.

Aliwataka wanafunzi hao kuwa mstari wa mbele kuielekeza jamii juu ya umuhimu wa sensa ili washiriki zoezi hilo katika maeneo husika ambayo watakuwapo.

"Ninaomba msaidie serikali kuwa mabalozi wazuri wa kuelimisha umuhimu wa Sensa ya Watu na Makazi tunahitaji kuona watu wanahesabiwa ili kusaidia serikali namna ya utekelezaji kiuchumi," alisema Kipanga.

Alisema sensa ya watu na makazi ina umuhimu kwa taifa kwa sababu inaisaidia serikali kupanga mipango mbalimbali ya maendeleo ikiwamo kujua idadi ya watu, jambo linaloiwezesha serikali kupeleka huduma katika maeneo hayo hususani za afya.

Mkurugenzi wa taasisi inayojishughulisha na utafiti wa kupunguza umaskini (REPOA), Dk. Donald Mmari, alisema mdahalo wa kutathmini miaka 60 ya uhuru na ushirikiano kati ya Tanzania na Marekani utalenga kuangalia uhusiano na ushirikiano katika miaka mingine 60 ijayo.

Alisema katika mdahalo huo eneo kubwa ni elimu, kukuza stadi na umahiri wa vijana ili washiriki katika uzalishaji ambao utasaidia kukuza maendeleo ya nchi.

Alisema midahalo kama hiyo tayari imefanyika katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Chuo Kikuu cha Mtakatifu Augustine (SAUTI), Nelson Mandela na UDOM.

Alisema REPOA kama taasisi ya utafiti imeshirikiana na Serikali ya Marekani kufanikisha mambo hayo kwa kushirikisha wanafunzi ili kutoa maoni yao kwenye kuimarisha sekta hiyo ya elimu, ambapo vijana watanufaika.

# Mkurugenzi akiri makosa kutaka kuvivunja vibanda

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MKURUGENZI wa Jiji la Dodoma, Joseph Mafuru, amebadili uamuzi wake wa kutaka kuvunja vibanda na kuwahamisha wafanyabiashara zaidi ya 7,000 wa Soko la Sabasaba jijini baada ya kukiri walikosea kutaka kufanya hivyo bila kuwashirikisha.

Mafuru alitangaza nia ya jiji hilo kuvunja soko hilo ifikapo Julai mwaka huu kwa kile kilichodaiwa kufanya maboresho ili kuwa na soko zuri lenye ubora unaokidhi mahitaji ya makao makuu ya nchi.

Akizungumza kwenye mkutano na wafanyabiashara wa soko hilo juzi, alikiri kuwa wao kama serikali walikosea kutangaza kuvunjwa kwa soko kabla ya kuzungumza na wafanyabiashara hao.

"Mmeongea vitu vingi vyenye maana na kufikirisha, tunapata mambo mengi kwenye maneno yenu, lakini mnapoongea mjue licha ya kwamba sisi ni viongozi hatujatoka mbinguni.

"Mfano mimi nimesomeshwa kwa pesa ya vitumbua, tunaishi maisha haya siyo ya kusimuliwa, hivyo serikali lazima tuseme kuna sehemu tulijikwaa," Mafuru alikiri kukosea.

Alisema wazo la serikali lilikuwa jema kwa kutaka soko hilo liwe la kisasa, wafanyabiashara wafanye shughuli zao na wateja wafanye ununuzi katika mazingira mazuri pamoja na kuweka huduma zote muhimu.

Alisema kuwa kabla ya kutangaza kuvunjwa kwa soko hilo, ilipaswa serikali ikae na wafanyabiashara kwa lengo la 'kuyajenga' ili kuweka uelewa wa pamoja.

"Ilikuwa serikali tukae na ninyi tujue changamoto ndipo tukae tuongee na media (vyombo vya habari) kuhusu kuvunjwa kwa soko hili lakini kwa hali ilivyo sasa, hatuwezi kuvunja soko hili," alifafanua.

Alisema katika kusudio la kufanya maboresho ya soko hilo, inabidi itengenezwe timu ya pamoja baina ya viongozi wa jiji na wafanyabiashara hao.

"Jiji la Dodoma linakusudia kufanya maboresho makubwa ya soko hili la Sabasaba, sasa tunatekelezaje? Ni suala la jiji na watu wa Sabasaba kutengeneza timu ya maboresho ya soko hili," alisema.

Aliongeza: "Wazo ni zuri sana, Dodoma ni makao makuu ya nchi, inapokea wageni na mji unazidi kukua lakini Sabasaba haifanani na makao makuu.

"Wakati wa mvua njia hazipitiki, watu wanauza mboga, nyanya, matunda yakiwa chini lakini maofisa afya wamekuwa wakiwaacha mfanye biashara japo haistahili. "Kwa hiyo, nikaandika barua kwa viongozi wa soko ili tufanye uhakiki kwa lengo la kujua nani yuko wapi, anafanya biashara gani na wakati wa kipindi cha ujenzi atakwenda kufanya biashara wapi ili kutupa mwelekeo wa nini cha kufanya wakati ujenzi unaendelea na wafanyabiashara wakiendelea na shughuli zao," alifafanua.

Mwenyekiti wa soko hilo, Athuman Makole, alisema wafanyabiashara hao waliingia katika soko kuanza kufanya shughuli zao kwa wito wa Rais wa awamu ya tatu, Benjamini Mkapa, baada ya kuvunjwa kwa soko lililokuwapo kipindi hicho katika viwanja vya Nyerere Square.

Mfanyabiashara Shukrani James alidai watu wengi sasa wamepata shinikizo la damu kutokana na soko hilo kutaka kuvunjwa na jiji.

Mfanyabiashara Adam Abdallah alisema wamefajirika kwa mkurugenzi kufuta uamuzi wake wa awali na kukubali kwenda kuzungumza nao ili ajue kero zao.



Naibu Meya wa Jiji la Dodoma, Emmanuel Chibago (kulia), akimpongeza Mkuu wa Idara ya Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika wa Jiji hilo, Yustina Munishi, baada ya kumkabidhi pikipiki 25 kwa ajili ya maofisa ugani wa jiji jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# TAMISEMI yamulika maficho hoja za ukaguzi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KATIBU Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Prof. Riziki Shemdoe, amezitaka halmashauri zote 184 nchini kuhakikisha zinatekeleza na kusimamia miradi yote inayopelekwa katika maeneo hayo ili kuepuka hoja za ukaguzi zinazotokea pindi miradi hiyo inaposhindwa kutekelezwa kwa wakati.

Akizungumza na wakurugenzi na maofisa ununuzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa juzi jijini Dodoma, alisema hoja za ukaguzi zinazotokea katika halmashauri zinaepukika na inawezekana kutokuwapo kabisa ikiwa watendaji watasimamia, kutekeleza majukumu yao na kufuata sheria na taritibu za utekelezaji wa miradi yote ya maendeleo inayopelekwa katika maeneo yao.

Alisema mpango wa utekelezaji unaowekwa na halmashauri husika katika utekelezaji wa miradi kisha kutokutekeleza au kubadilisha matumizi ya malengo yaliyowekwa na kutofuata sheria, ni miongoni mwa vyanzo vikubwa vya hoja za ukaguzi.

"Pesa za ruzuku zinazopelekwa halmashauri kubadilisha matumizi kwa kutokuomba kibali vinachangia hoja hizi.

"Watendaji wenzangu tufuateni sheria kuepuka hoja, tufuate taratibu za kazi, sisi kama viongozi na ni watendaji, tushirikianeni ili tumalize hoja hizi," aliagiza.

Prof. Shemdoe pia aliwaelekeza wakurugenzi wote kuisimamia miradi inayopelekwa kwenye maeneo yao kwa ubora na wahakikishe thamani ya fedha inaonekana.

Mwenyekiti wa wakurugenzi hao, Kiomoni Kibamba, aliishukuru serikali kwa kuendelea kupeleka miradi ya maendeleo na kuahidi wataendelea kuisimamia kwa kuzingatia maelekezo wanayopatiwa.

"Kupitia kikao hiki cha tathmini ya utendaji wa miradi ya maendeleo, tunaahidi tutaendelea kufanya kazi kwa uadilifu na ubora unaotakiwa ili wananchi wapate huduma bora," alisema Kibamba.

Kikao hicho cha siku moja kilikuwa na lengo la kujadili tathmini ya utekelezaji wa miradi ya UVIKO-19 na miradi mingine yote inayotekelezwa kwenye halmashauri nchini.



# UWT kujenga nyumba

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JUMUIYA ya Umoja wa Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (UWT) Mkoa wa Mbeya inatarajia kutumia Sh. milioni 48 kujenga nyumba.

Ujenzi wa nyumba hiyo ni sehemu ya mradi wa ujenzi wa nyumba za kupangisha ambazo zitakuwa sehemu ya vitega uchumi vya jumuiya hiyo.

Hayo yalibainishwa na Katibu wa UWT Mkoa wa Mbeya, Mary Mwasengo, alipokuwa anapokea msaada wa matofali 3,000 kutoka kwa Mkurugenzi wa Shule za Patrick Mission ya mkoani Dar es salaam na Paradise Mission ya mkoani Mbeya.

Alisema nyumba hizo zitajengwa kwenye uwanja wao uliopo katika eneo la Forest Mpya, kwamba kwa kuanzia wanajenga nyumba moja ambayo itakuwa inakaliwa na familia mbili.

Mwasengo alisema uwanja wao una ukubwa wa zaidi ya mita 3,000 na kwamba mbali na nyumba za kupangisha pia watajenga nyumba ya kuishi Katibu wa Jumuiya hiyo.

Alisema kutokana na msaada wa tofali walioupata mradi wa nyumba hiyo utakamilika haraka kwa sababu vifaa vyote vya ujenzi vipo tayari, kwamba mfadhili ameahidi kuwapeleka mafundi wake wanaojenga miradi ya shule zake.

"Ili kukamilisha mradi huu, tumeamua wote tuchangie kwa kuanzia kwenye mashina, kata na sisi wajumbe wa sekretarieti ambapo wenzetu wa mashina tumewataka wachangie Sh. 3,000 kila shina, Sh.5,000 kila kata na sisi wajumbe wa sekretarieti tumekubaliana kuchangia Sh. 20,000," alisema Mary. Akikabidhi msaada huo, Mwaselela ambaye ni miongoni mwa wadau wa maendeleo wa Mkoa wa Mbeya, alisema mbali na kuchangia matofali hayo pia atagharamia ujenzi wa mradi huo kuanzia chini mpaka kwenye hatua ya uwezekaji.

Mwaselela alisema pia atawatumia mafundi wake ambao huwa anawatumia kwenye ujenzi wa shule zake kujenga mradi huo, ili kuupunguzia umoja huo gharama za ujenzi wa mradi pamoja na kuharakisha ukamilishaji.

Alisema awali aliahidi kutoa Sh. milioni 10 lakini kutokana na sababu mbalimbali aliamua kubadilisha na kuanza kutoa vifaa na kwamba atahakikisha vifaa anavyovitoa vinafikia thamani ya fedha alizoahidi.

Mwaselela alisema endapo ujenzi utakamilika kwa wakati bado vifaa havijafikia thamani ya fedha alizoahidi atawakabidhi wahusika.

"Mimi pamoja na taasisi zangu tutahakikisha tunakuwa bega kwa bega na jumuiya hii ili kuhakikisha inafanikiwa, fedha hizi tunazotoa ni sehemu ya faida ambayo tunapata kwenye taasisi zetu na kinamama ni miongoni mwa taasisi muhimu sana kwetu," alisema Mwaselela.

Hata hivyo aliipongeza jumuiya hiyo kwa kubuni mradi huo akisisitiza kuwa utawasaidia kuwa na uchumi ambao utakuwa wa kujitegemea na kuwaondolea adha ya kuwa ombaomba.

Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha ya UWT Mkoa wa Mbeya, Edna Mwaigomole, alimshukuru Mwaselela kwa msaada huo na kumtaka kutochoka kuisaidia UWT na badala yake aendelee kutokana na kuwa na uwezo mdogo.



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera (wapili kushoto), akiandika madaraja ya tumbaku ya wakulima, wakati alipokuwa anazindua masoko ya tumbaku katika mkoa wa kitumbaku wa Chunya, kwenye ghala la Chama cha Msingi cha Wakulima wa Tumbaku Bitimanyanga hivi karibuni. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wahitaji sheria ndogo kumaliza ukatili kijinsia

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

HALMASHAURI ya Wilaya ya Rungwe mkoani Mbeya imewaomba wadau hasa taasisi za msaada wa kisheria kwenda kusaidia wananchi katika vijiji vya halmashauri hiyo kupata sheria ndogo ambazo zitawawezesha kumaliza migogoro ya ardhi na ukatili wa kijinsia.

Ombi hilo lilitolewa juzi na viongozi wa idara za sheria na maendeleo ya jamii mbele ya wadau wanaotekeleza mradi wa mwanamke imara unaolenga kuwapatia wananchi msaada wa kisheria na kukabiliana na ukatili wa kijinsia.

Mradi huo unatekelezwa nchini kwa ufadhili wa Shirika la Misaada la Watu wa Marekani (USAID) na wilayani Rungwe linaendelea katika Kata ya Kiwira, Kisondela na Masoko ambako wananchi wanapewa msaada wa kisheria.

Akizungumza mbele ya wadau hao, Ofisa Maendeleo katika Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe, Pongezi Sanga, alisema katika wilaya hiyo kuna migogoro mingi ya kijamii ambayo inahitaji uwapo wa sheria ndogo ili kukabiliana nayo.

"Katika wilaya yetu kuna migogoro mingi, lakini migogoro inayoongozwa kwa kuripotiwa ni ile ya ardhi na ukatili wa kijinsia, hivyo tunahitaji wananchi vijijini wasaidiwe kuandaa sheria ndogo ambazo zitawawezesha wao wenyewe kukabiliana na migogoro hiyo na ikibidi kuimaliza kabisa," alisema Sanga.

Alisema katika maeneo ambayo mradi huo unatekelezwa migogoro hiyo imepungua kwa kiwango kikubwa kutokana na wananchi kuwezeshwa kupata sheria ndogo zinazowaongoza kwenye maeneo yao.

Mwanasheria wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe, Richard Pondo, alisema idadi kubwa ya vijiji wilayani Rungwe havina sheria ndogo hali ambayo inasababisha kuwapo kwa migogoro mingi inayoripotiwa kwenye vyombo vya dola.

Pondo alisema mchakato wa kuandaa sheria ndogo vijijini unahitaji gharama kubwa kiasi kwamba kutokana na ufinyu wa bajeti halmashauri haiwezi kuwawezesha wananchi wa vijiji vyote kupata sheria ndogo kwa wakati.

"Sisi kama halmashauri tunashindwa kuwasaidia wananchi wa vijiji vyote kupata sheria ndogo kutokana na ufinyu wa bajeti, ingawa tumeanza katika vijiji vichache lakini hatuwezi kuwafikia wote kwa wakati, hivyo ikiwezekana tunaomba wadau watusaidie katika hili," alisema Pondo.

Alisema kuwa vijiji vingi vina sheria chache ambazo zimepitwa na wakati, hivyo mchakato huo ni muhimu ukafanyika ili kuwasaidia wananchi kupata sheria mpya na kuboresha zile za zamani.

Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii Wilaya ya Rungwe, Omary Mungi, aliwataka wadau wanaofika wilayani Rungwe kwa lengo la kuelimisha au kutekeleza miradi mbalimbali kwa wananchi kuwatumia watu maarufu na wale wenye ushawishi mkubwa ili waweze kufanikiwa.

Aliwataja watu hao wenye ushawishi kwenye Jamii ya wananchi wa Rungwe kuwa ni viongozi wa dini, wazee wa mila maarufu kama machifu na viongozi wa vijiji.

"Hapa wilayani Rungwe kuna watu ambao wanaaminiwa na wananchi kuwa ndiyo chachu ya mabadiliko, unapokuja kufanya jambo lolote ili ufanikiwe ni muhimu ukawaona hao, vinginevyo hautafanikiwa kwa kiwango kikubwa," alisema Mungi.

# 'Wanafunzi wa vyuo vikuu wawe wabunifu'

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAZIRI wa Elimu na Taaluma wa Serikali ya Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST), Albert Chami amewashauri wanafunzi wa shule za msingi mpaka vyuo vikuu kujikita kwenye masuala ya ubunifu.

Amesema ubunifu huo unatakiwa uanzie kwenye nyanja za sayansi na teknolojia, kibiashara na ujasiriamali.

Alitoa ushauri huo wakati akizungumza kwenye ufunguzi wa Wiki ya Ubunifu kwa Mkoa wa Mbeya, yenye kauli mbiu isemayo 'Ubunifu kwa maendeleo endelevu', inayofanyika katika Chuo Kikuu cha MUST kilichoko eneo la Iyunga jijini Mbeya.

Chami alitoa wito kwa wanafunzi na wanazuoni wote mkoani humo, kuhakikisha wanatembelea kwenye mabanda yaliyoko kwenye wiki hiyo ya ubunifu, kwani kuna mambo mengi ya kujifunza na hivyo kupata ufahamu na fursa zaidi.

"Kwani maisha ya sasa kila kitu kinahitaji kuwa na ubunifu, yaani kwenye taasisi zetu, elimu na kila kitu hivyo ni vyema ubunifu upewe zaidi kipaumbele zaidi," alisema Chami.

Alisema MUST kupitia moja ya idara yao, inao utaratibu wa kuwasaidia wabunifu, kwamba huwa inawapika katika sekta zao ambazo wamejikita na wabunifu hao siyo lazima wawe wanachuo kwani hata walio nje ya chuo hicho huwa wanawasaidia.

Mwanafunzi wa kidato cha tano katika Sule ya Sekondari Iyunga, Asajile Mwaipopo, alisema wamepata nafasi ya kushiriki kwenye wiki hiyo ya ubunifu, kwamba wameweza kujifunza mambo mengi, huku wakitambua ubunifu ni moja ya sehemu kubwa katika maisha ya binadamu.

Mwaipopo alisema ubunifu huwa unawasaidia wanafunzi kutambua kuwa wakiutumia vizuri wanaweza kujiajiri.

Kaimu Mkurugenzi wa Kitivo cha Ubunifu na Uhaulishaji wa Teknolojia MUST, Dk. Juma Mpangule, alisema moja kati ya vitengo vilivyo chini ya kitivo hicho, kiitwacho ubunifu na uatamizi ndiyo kimeratibu shughuli hiyo.

Dk. Mpangule aliongeza wao kama waangaliaji wa hilo, wameenda kuona jinsi wanavyoweza kushiriki, lakini vile vile kufikisha ujumbe kwa wananchi, kwamba MUST sasa hivi inao utaratibu kwa ajili ya kupokea wabunifu na wajasiriamali.



## Kilimo cha umwagiliaji kuimarishwa Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI imesema imejipanga kuimarisha sekta ya kilimo cha umwagiliaji ili Zanzibar inajitosheleza kwa chakula, ikianza mazungumzo na Benki ya Korea Kusini ili kupata mkopo wa dola za Marekani milioni 18.9 kwa ajili ya kilimo hicho.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango, Dk. Saada Mkuya Salum, alibainisha hayo jana alipotoa ufafanuzi wa michango ya wajumbe wa Baraza la Wawakilishi waliochangia bajeti hiyo katika eneo la kilimo na kujitosheleza kwa chakula.

Alisema miongoni mwa mikakati ya serikali katika bajeti yake ni kuendeleza sekta ya kilimo cha umwagiliaji ili Zanzibar ijitegemee kwa chakula.

Alisema kuwa katika bajeti, sekta hiyo inachukua asilimia 36 katika kufidia gharama za uingizaji wa chakula ikiwamo mchele ambao ndiyo maarufu unaotumiwa na wananchi wengi katika matumizi ya kila siku.

Dk. Mkuya alisema kilimo cha umwagiliaji maji kimeonekana ndiyo mkombozi kwa wakulima kufuatia kuwapo kwa mabadiliko ya tabia ya nchi na uhaba wa mvua zinazobadilika katika msimu mbalimbali.

Alisema serikali ipo katika mazungumzo na Benki ya Korea Kusini ombi la mkopo wa dola za Marekani milioni 18.9 kwa ajili ya maendeleo ya mradi wa umwagiliaji maji kwenye Bonde la Cheju B Wilaya ya Kati Unguja.

Aliyataja mabonde mengine ambayo yamepewa kipaumbele ikiwamo ujenzi wa miundombinu ya njia za kusafirisha maji kuwa ni pamoja na Mtwango Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Katika mradi huo utahusisha uchimbaji wa visima kwa ajili ya kuzalisha maji mengi yatakayotumika katika usambazaji wa maji mashambani.

"Mheshimiwa Spika, ninataka niwaambie wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba tumejipanga kuona tunajikita moja kwa moja katika kuimarisha kilimo cha umwagiliaji maji ili tujitosheleze na chakula na kukigeuza kuwa cha biashara zaidi," alisema.

Dk. Mkuya pia alisema serikali inafuatilia kwa karibu fedha za mkopo kutoka Shirika la Kimataifa la Korea Kusini (KOICA) kwa ajili ya kusaidia maendeleo ya mazao ya baharini ikiwamo mwani na majongoo ya baharini, yakinufaisha zaidi wanawake. Alisema miongoni mwa ahadi za Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi ni kuwaendeleza wanawake wanaoishi katika maeneo ya pembezoni mwa fukwe katika kujikita kwenye kilimo cha mwani na mazao ya baharini.

Alisema tayari serikali ipo katika mchakato wa kujenga kiwanda cha kuongeza thamani zao hilo ili kuleta mabadiliko makubwa ya kiuchumi kwa wanawake ambao kwa asilimia 84 wanalima kilimo hicho vijijini.




Mhamasishaji wa uhifadhi wa mazingira wa kisiwa cha Chumbe, Khamis Khalfan Juma (katikati), akizungumza na waandishi wa habari, kuhusu uhifadhi wa mazingira kisiwani humo, Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Huduma za benki sasa kupelekwa Z'bar vijijini

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

BENKI ya Watu wa Zanzibar (PBZ) imesema imejipanga kusogeza huduma za kibenki hadi vijijini ili kuleta mabadiliko makubwa na kufikisha huduma za kifedha na kiuchumi kwa wananchi wote.

Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango, Ali Suleiman Ameir, alibainisha hayo jana wakati akitoa ufafanuzi wa shughuli za PBZ katika kufikisha huduma zake na kwenda na ushindani wa kibenki.

Alisema kwa mwaka wa fedha 2022/23, PBZ inakusudia kufungua vituo vya kutolea fedha huko Gombani, Konde, Mtambile kwa upande wa Pemba.

Alisema vituo kama hivyo vinatarajiwa kujengwa huko Marumbi Wilaya ya Kati, Tunguu, Dunga na Nungwi Mkoa wa Kaskazini Unguja, akisisitiza kuwa kwa kiasi kikubwa vitawapunguzia wananchi safari kwenda mjini kutafuta huduma hizo.

Alisema uongozi wa benki hiyo umeweka mikakati ya kufungua huduma za kibenki katika mikoa hiyo baada ya kufanya utafiti na kubaini kuongezeka kwa shughuli za kifedha zinazotokana na kuongezeka kwa biashara.

"Mheshimiwa Spika, Benki ya Watu wa Zanzibar imejipanga kusogeza huduma zake za kibenki karibu na wananchi ili kusaidia kukuza uchumi na maendeleo katika mzunguko wa fedha," alisema.

Akifafanua zaidi kuhusu kuimarika kwa huduma za kibenki, Ameir alisema PBZ imepiga hatua kubwa ambapo kwa sasa mtaji wake unatarajiwa kukua kwa asilimia 16 kutoka Sh. bilioni 122 hadi kufikia Sh. bilioni 146.

Alisema benki hiyo inatarajiwa kupata faida Sh. bilioni 35.54 kwa mwaka 2022 kulinganisha na faida ya mwaka 2021 ya Sh. bilioni 22.69, sawa na ongezeko la asilimia 57.

# Serikali yasaka fedha ujenzi barabara vijijini

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema imeanza mchakato wa kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya barabara za vijijini kwa ajili ya kufikia malengo ya uwekezaji na uchumi na uimarishaji wa sekta ya utalii nchini.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango, Dk. Saada Mkuya, aliyasema hayo wakati akijibu hoja za wajumbe wa Baraza la Wawakilishi waliochangia makadirio mapato na matumizi ya bajeti ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2022/23.

Dk. Mkuya alisema Zanzibar inatarajia kupata fedha za mkopo za Euro milioni 460 kutoka katika mfuko wa kuhamasisha biashara wa Uingereza kwa ajili ya kutekeleza miradi ya kimkakati ya miundombinu. Aliitaja miradi ya miundombinu ya barabara zenye urefu wa kilomita 103.5 zinatarajiwa kujengwa Unguja na Pemba, hatua ambayo itasaidia kuimarisha mawasiliano katika sekta za kilimo na utalii.

Alizitaja barabara zinazotarajiwa kujengwa ikiwamo Tunguu hadi Makunduchi yenye urefu wa kilomita 48, Fumba hadi Kisauni yenye urefu wa kilomita 12, mkoani hadi Chakechake Pemba yenye urefu wa kilomita 43.5.

Alisema barabara ya Chakechake hadi Mkoani ni miongoni mwa barabara za kimkakati ambayo ujenzi wake utaiunganisha mikoa miwili ya Kisiwa cha Pemba ikiwamo katika maeneo huru ya Micheweni, Pemba.

"Mheshimiwa Spika, barabara ya Chake Chake hadi Mkoani ni muhimu ambayo imelenga kuiunganisha mikoa miwili ya Kisiwa cha Pemba pamoja na maeneo ya uwekezaji ya Micheweni ikiwa ni sehemu ya mikakati ya kukifungua Kisiwa cha Pemba kiuchumi," alisema.

Vilevile, alisema katika ujenzi wa miundombinu, Serikali ya Zanzibar imeweka mikakati ya ujenzi wa uwanja wa ndege wa Pemba ikiwa ni juhudi za kukiunganisha Kisiwa cha Pemba na sekta ya utalii.

"Mheshimiwa Spika majadiliano ya upatikanaji wa mkopo wa fedha hizo yanaendelea kupitia kamati ya madeni ya kitaifa (NDMC) ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania," alisema.

Baadhi ya wajumbe wa Baraza la Wawakilishi waliitaka serikali kuanza kutekeleza mradi wa ujenzi wa uwanja wa ndege wa Pemba pamoja na kulipa fidia kwa wananchi waliopisha ujenzi huo.

Mwakilishi wa Mtambwe, Habib Mohamed, alisema ujenzi wa uwanja wa ndege wa Pemba ni muhimu katika mikakati ya kukifungua kisiwa cha Pemba kiuwekezaji pamoja na sekta ya utalii.

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

1FORM 58

**IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE**
**AT ONE STOP CENTRE**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE**
**NO.361 OF 2022**

**In The Matter Of the Estate of the Late.................BENITO TADEUS KIDASSI**
**And**
**In The Matter Of Application for Letters Of Administration by**
**LUDOVICK BENITO KIDASI**

**GENERAL CITATION**
**(RULE 75)**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of administration) is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 4th day JULY 2022

**Dated at DAR ES SALAAM this 11th day of MAY 2022**

Registrar/Senior Resident Magistrate

## PASSPORT IMEPOTEA



**NDUGU PAUL MICHAEL NANDRIE** anatangaza kupotelewa na passport yake yenye No. AB772882 iliyotelewa 20th, November,2015 na muda wake wa kuisha ni 19, November,2025. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi: **Taarifa ya Polisi DSM/PHQ/RB/199827 /2022.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**BARAKA PATRICK SAMILA** anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili **MC 938 BFM** Eng. namba **KL157 MI 16j02582** Card namba **7370326** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa polisi **Taarifa ya polisi RB. Namba IRI/IRI/RB/177799/2022**

## KUPOTEA KWA VYETI



**DANIEL CHARLES LYIMO** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.0328/0131 kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **MAWENZI SECONDARY SCHOOL** mwaka 2013 na cheti cha kidato cha sita chenye index namba S.1600/0516 kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupiyia **BISHOP DURNING HIGH SCHOOL mwaka 2016** . kwa yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo cha polisi.

**POLISI TAARIFA: SIN/SIN/RB/22596/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**DODOMA KILIMO LIMITED** anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye namba za usajili **T922BUJ** aina ya Scania, Chasis **No.4457930,** Engine **No.6143864.** yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. **Taarifa ya polisi DOD/DOD/RB/228632/2022**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo Wilaya ya MOROGORO**
**Kituo cha MJINI Mkoa Wa MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi Na......26 /2022**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU: WILBROAD THADEO NGOMALUFU WA MAWEZI**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA: AZIZA KONDO NASSORO**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5 (2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 27 Mwezi 06 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**

- Endapo kuna yoyote mwenye wosia na marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia ya narehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.
- Marehemu hakuacha wosia
- Futa isiyohusika.

**Imetolewa Tarehe 25 Mwezi 05 Mwaka 2022**

**HAKIMU**


Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

KWA HABARI MOTOMOTO USIKOSE GAZETI LAKO LA NIPASHE KILA SIKU

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharasma yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## Waonywa kupeleka wagonjwa kwa waganga wa tiba za asili

**Na Happy Severine,** BARIADI

WANANCHI wa Kata ya Nkololo na maeneo jirani wametakiwa kuacha tabia ya kuwapeleka wagonjwa katika zahanati bubu na waganga wa tiba asilia, badala yake wawawahishe katika hospitali zilizoko jirani ili kupata matibabu stahiki.

Wito huo umetolewa jana na Paroko wa Parokia ya Nkololo Padri Paul Fagan katika misa takatifu ya kuadhimisha miaka 62 ya upadri wake iliyofanyika viwanja vya kituo cha afya cha Nkololo.

Padri Fagan alisema wakazi wengi wa maeneo hayo wamekuwa wakiwapeleka wagonjwa wao kwa waganga wa tiba asilia na katika zahanati bubu.

Alisema kwamba mara nyingi hushindwa kutibika na mwishoni kukimbizwa katika Kituo cha Afya cha Songambele wakiwa na hali mbaya na hatua ya mwisho ambayo wengi wao upoteza maisha pindi wanapofikishwa hospitalini hapo.

Padri Fagan alisema ni vema wananchi wakaacha imani potofu na pindi wapatapo mgonjwa wampeleke hospitali ili waweze kupatiwa vipimo na matibabu sahihi kwao.

"Wagonjwa wengi wanaletwa katika kituo chetu cha afya cha Songambele ambacho kwa sasa kimepata adhi ya kuwa hospitali wakiwa katika hali mbaya zaidi...na wengi wanaoletwa wakiwa katika hatua za mwisho na hii inatupa wakati mgumu kupigania uhai wao wakiwa mahututi...hivyo niwashauri wananchi waache kuanza na matibabu ya pembeni na ya siri yasiyo na vipimo," alisema Padri Fagan.

Alisema alipofika katika kata hiyo wakati wa kuhubiri imani aliamua kujenga kituo hicho cha afya ili wananchi waache kwenda kwa waganga wa kienyeji kupata matibabu.

Aliongeza kuwa ni matumaini yake kupitia injili inayotolewa makanisani wananchi na waumini wa kanisa hilo watazingatia suala la matibabu sahihi yenye vipimo.

Sambamba na hilo, Padri Fagan aliahidi kufanya harambee ya kuchangia ujenzi wa chuo cha wauguzi kitakachojengwa karibu na Kituo cha Afya cha Songambele ili kuhakikisha wanapatikana wataalamu wengi wa afya ambao watakwenda kusaidia jamii kupata matibabu sahihi.

Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, David Kafulila, alimpongeza Padri Fagan na kuahidi kutoa ushirikiano wa karibu wakati wa harambee ya ujenzi wa chuo hicho.

Kafulila alisema suala la imani kwa kila mwanadamu ni la msingi na kwamba kila muumini wa madhehebu tofauti wanapaswa waishi kwa kumtegemea Mungu ili kuleta amani na utulivu wa nchi.

Mbunge wa Bariadi, Kundo Mathew alisema hapo awali tatizo kubwa ilikuwa ni uhaba wa zahanati na hospitali lakini kwa sasa kila sehemu ina huduma hizo.

Mhandisi Kundo alieleza kuwa katika maeneo mengi ya Bariadi Padri Fagan amekuwa msaada mkubwa kwa wakazi wa huko, kwani amesaidia suala la barabara, elimu na huduma za afya.

# Mbaroni tuhuma kuua mume kwa kumkaba

**Na Halima Ikunji,** TABORA

JESHI la Polisi mkoani Tabora linamshikilia Maria Matheo kwa tuhuma za kumuua mume wake, Gabriel Nguwa (80), kwa kumkaba shingoni akiwa amelala.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tabora, Richard Abwao, akizungumza na waandishi wa habari jana mkoani hapa, alisema tukio hilo lilitokea Mei 30 mwaka huu.

Alisema kwamba mnamo tarehe tajwa, majira ya saa nane usiku , kulitokea tukio la mauaji hayo katika Kitongoji cha Bugwed, Kijiji cha Budushi, Kata ya Budushi wilayani Nzega mkoani Tabora.

Kamanda huyo alisema chanzo cha mauaji hayo ni mgogoro wa muda mrefu kati ya wanandoa hao hususani nyakati za jioni, mke anapolewa alikuwa nakumtumu mumewe kuwa hakuwa na msaada wowote katika maisha yao.

Kamanda Abwao alisema kwamba mbinu iliyotumika ni kumvizia mume akiwa amelala na kumkaba shingoni na kusababisha kifo.

Aliendelea kuwaeleza waandishi wa habari kwamba katika kipindi cha mwezi Mei mwaka huu, jeshi hilo lilifanya msako na kuwakamata watuhumiwa 71 kwa makosa mbalimbali.

Alisema kwamba kati yake, makosa ya mauaji walikamatwa watuhumiwa 19, wizi watuhumiwa 31, watuhumiwa wa uvunjaji ni 17 na watuhumiwa wanne wa makosa ya kubaka.

Alisema jeshi hilo pia liliwakamata waganga wawili wasiokuwa na vibali katika Kitongoji cha Lugange, Kijiji cha Gilimba, Kata ya Igulungu Wilaya ya Uyui mkoani Tabora.

Kamanda Abwao aliwataja waganga hao kuwa ni Yunge Kija (25) na Bundi Makomango (29) na kuongeza kuwa mnamo Mei 31 mwaka huu, majira ya saa tatu asabuhi katika Kijiji hicho, waliwakamata watu hao wakifanya shughuli za uganga wakiwa hawana vibali vya kufanyia kazi hiyo.




Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu (UNFPA) Tanzania, Mark Bryan Schreiner (kulia), akizungumza na waandishi wa habari, baada ya ukaguzi wa ujenzi wa jengo la kituo cha pamoja cha kuhudumia waathirika wa ukatili wa kijinsia kinachojengwa, Kata ya Bugarama wilayani Kahama, mkoani Shinyanga jana. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Adaiwa kuua mpenzi wake kisha kujiua kwa sumu

**Na Maulid Mmbaga**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam limesema linafanya uchunguzi wa tukio la mauaji lililofanywa na Bunanza Manyanda (34), mkazi wa Charambe wilayani Temeke anayedaiwa kumuua rafiki yake wa kike kisha yeye kujiua.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Kamanda wa Kanda Maalum, Jumanne Muliro, Manyanda anadaiwa kumuua kwa kumchoma na kitu chenye ncha kali tumboni rafiki yake Happiness Zakaria (23), mkazi wa Mbagala Charambe.

Suala hilo limetokea ikiwa ni siku chache baada ya tukio la mauaji ya wanandoa lililotokea mkoani Mwanza la kijana Said kudaiwa kumuua kwa kumpiga risasi mkewe, Swalha kutokana na kile kilichodaiwa wivu wa mapenzi.

Kamanda Muliro alibainisha kuwa baada ya mtuhumiwa Manyanda kufanya mauaji hayo, alijiua kwa kunywa sumu ya kuulia wadudu wa mazao inayojulikana kama Dudu Cron ambayo aliichanganya na pombe.

"Chanzo kilichosababisha kutokea kwa matukio yote mawili bado kinachunguzwa, na miili ya marehemu hao imehifadhiwa Hospitali ya Taifa Muhimbili kwa hatua zaidi," alisema Kamanda Muliro.

# HATIMA YA JKT LIGI KUU SASA JULAI 13

**Na Adam Fungamwango**

HATMA ya JKT Tanzania kupanda Ligi Kuu Tanzania Bara, sasa itajulikana Julai 13, itakapochezwa mechi ya pili ya mchujo 'play off' kati ya timu hiyo na mshindi wa 13 au 14 wa Ligi Kuu.

Kwa mujibu wa ratiba iliyotolewa jana na Bodi ya Ligi, ni kwamba timu zilizomaliza nafasi ya 13 na 14 kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara ambazo mpaka sasa hazijajulikana, zitacheza mechi ya kwanza ya mchujo Julai 3 na marudiano yatakuwa ni Julai 6.

Katika taarifa hiyo, Bodi ya Ligi imesema mshindi wa jumla kati ya timu hizo mbili kati ya aliyeshika nafasi ya 13 au 14, atakwenda kucheza mechi nyingine ya mchujo dhidi ya JKT Tanzania Julai 9, na mechi ya marudiano itakuwa Julai 13.

JKT Tanzania imepata nafasi ya kucheza 'play off' hivi karibuni, baada ya kuifunga Kitayosce FC kwenye mechi nyingine ya mchujo kwa timu za Ligi ya Championship, ikishinda mabao 2-0 nyumbani, kabla ya kulazimisha sare ugenini ya bao 1-1 kwenye mechi ya marudiano, hivyo kushinda kwa jumla ya mabao 3-1.

Iwapo JKT Tanzania itashinda kwenye matokeo ya jumla ya mechi hiyo itapanda na kuungana na Ihefu na Singida Big Stars kucheza Ligi Kuu msimu ujao, lakini ikifungwa itabakia kwenye Ligi ya Championship.

Nayo timu iliyotoka Ligi Kuu ikishinda mechi hiyo itasalia huko, lakini ikipoteza kwenye mechi hizo za mchujo itashuka daraja.



Vijana wakicheza mpira wa magongo katika viwanja vya Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Kapama afunguka kuhusu hatima yake

**Na Saada Akida**

BAADA ya kuhusishwa katika rada za kuwaniwa saini yake na klabu ya Simba, kiungo wa Kagera Sugar, Nassoro Kapama amefunguka na kusema ataweka wazi ofa yake baada ya kumalizika kwa msimu huu wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Awali taarifa ilivuma kwamba, jina la Kapama limependekezwa na Pablo Franco Kocha aliyeondolewa Simba na nyota huyo kujadiliwa na kamati ya usajili ya klabu hiyo kwa ajili ya na kuona jinsi gani ya kupata saini yake.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kapama alisema hawezi kuweka wazi mipango ne ofa alizopata na hataweka wazi ni wapi atakwenda hadi hapo atakapomaliza mkataba wake mwisho wa msimu huu.

Alisema mbali na ofa zilizofikia kwake lakini anaipa kipaumbele Kagera Sugar kwa lengo la kuongeza mkataba kama wanahitaji huduma yake kuendelea kusalia ndani ya timu hiyo.

"Ofa ndiyo zipo zimekuja kwangu, lakini timu za hapa hapa nyumbani miongoni mwao na moja ya klabu kongwe hapa nchini imeonesha nia, ila siwezi kuweka wazi kila kitu kwa sababu bado niko na mkataba na waajiriwa wangu Kagera Sugar, unamalizika mwishoni mwa msimu huu," alisema Kapama. Alisema suala la wapi atakwenda bado hajajua kwa sababu bado anaipa nafasi timu yake ya Kagera ambayo bado wako katika kipindi kigumu katika mechi zilizopo mbele yao kuhakikisha wanamaliza vizuri msimu huu.

Kagera tayari iko Bukoba kwa ajili ya maandalizi ya michezo minne iliyosalia ya Ligi hiyo huku wanajiandaa na mchezo ujao dhidi ya Biashara United utakaopigwa Juni 14, mwaka huu katika dimba la Kaitaba.

## SHIMIWI kuchaguana Juni 17

**Na Shufaa Lyimo**

UCHAGUZI mkuu wa Shirikisho la michezo kwa Wizara pamoja na Idara za Serikali (SHIMIWI) unatarajiwa kufanyika Juni 17 mwaka huu mkoani Morogoro.

Akizungumza jijini jana Kaimu mkuu wa kitengo cha uhusiano na mawasiliano wa Baraza la Michezo Tanzania (BMT), Najaha Bakari alisema awali uchaguzi huo ilipangwa ufanyike Mei 25 mwaka huu, lakini ulisogezwa mbele kutokana na sababu maalumu.

"Uchaguzi huo utafanyika kwa kuzingatia kanuni ya SHIMIWI ya mwaka 2009 na kesho (leo) litaanza zoezi la kuchukua na kurudisha fomu za wagombea," alisema Najaha.

Najaha alisema nafasi ambazo zinawaniwa kwenye uchaguzi huo ni Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti, Katibu Mkuu, Katibu Mkuu msaidizi, mweka hazina, mweka hazina msaidizi, wajumbe watano wa Kamati ya utendaji pamoja na nafasi mbili za viti maalumu kwa upande wa wanawake.

Alisema usaili wa wagombea hao utafanyika Juni 16 mwaka huu ukifuatiwa na mkutano mkuu utakaofanyika Juni 17 mwaka huu, ikiwa ni siku moja kabla ya kufanyika kwa uchaguzi huo.

Vile vile alivitaka vyama pamoja na kamati za michezo kufanya uchaguzi huo Kwa mujibu wa katiba ikiwemo kulipa ada.

## Biashara yanolewa na Mkurugenzi

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kutimua benchi lote la ufundi kwa sasa timu ya Biashara United inanolewa na Mkurugenzi wa Ufundi wa klabu hiyo, Omari Madenge kuelekea kwenye mechi nne zilizosalia.

Hata hivyo kuna taarifa kuwa kocha wa zamani wa Mwadui, Khalid Adam huenda akaongezwa ili kuongeza nguvu kwenye benchi hilo.

Akizungumza kutoka mkoani Mara, Mkurugenzi huyo alisema kuwa wanaendelea na mazoezi kwa ajili ya kuivaa Kagera Sugar Juni 14, akisema lengo kubwa ni kuhakikisha timu inabaki Ligi Kuu.

"Lazima tuendelee na mazoezi kwa sababu tumebakisha mechi nne na lazima tupambane ili tushinde, ni muhimu sana. Kwa bahati mzuri vijana hawa wote nawafahamu na sasa wako chini yangu, tutafanya kile ambacho wana Mara wanakitaka ili tunusurike kuteremka," alisema Mkurugenzi huyo.

Naye nahodha wa timu hiyo, Ramadhani Chombo 'Redondo', amesema bado hawajakata tamaa kwa sababu kwa jinsi msimamo ulivyo ni juhudi tu za timu ndizo zitakazoibakisha.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### LUKAKU ARUHUSIWA
CHELSEA imemwambia mshambuliaji wao Mbelgiji, Romelu Lukaku mwenye umri wa miaka 29, anaweza kujiunga tena na Inter Milan kwa mkataba wa mkopo. ***(Guardian)***

### NUNEZ ANASITA
MSHAMBULIAJI wa Benfica, Darwin Nunez mwenye umri wa miaka 22, anasitasita kujiunga na Manchester United kwa sababu hawako katika Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao. ***(Mirror)***

### LIVERPOOL WAMEJIONDOA
LIVERPOOL wamejiondoa katika mbio za kuwania kumsajili nyota wa Benfica, Darwin Nunez mwenye umri wa miaka 22. ***(Star)***

### FOFANA AGOMBEWA
MANCHESTER United na Chelsea zinamwania mlinzi wa Leicester mwenye umri wa miaka 21, Mfaransa Wesley Fofana. ***(RMC Sport)***

### JUVE WASITISHA
JUVENTUS wamesitisha mpango wa kutaka kumsajili mshambuliaji wa zamani wa Manchester United, Jesse Lingard baada ya awali kutangaza nia ya kumsajili mchezaji huyo wa kimataifa wa England mwenye umri wa miaka 29. ***(Goal)***

### BALE NA GETAFE
MSHAMBULIAJI wa Wales, Gareth Bale mwenye umri wa miaka 32 anaweza kusajiliwa na Getafe yenye makao yake Madrid. ***(Mail)***

### WAKALA AKATAA
WAKALA wa Gareth Bale, Joshua Barnett ametupilia mbali kuwapo kwa uhusiano wowote baina ya mteja wake na klabu ya Ligi Kuu ya Hispania, Getafe. ***(Fabrizio Romano)***

### TIMBER AONYWA
KOCHA wa zamani wa Manchester United, Louis van Gaal amemwonya mlinzi wa Ajax na Uholanzi, Jurrien Timber mwenye umri wa miaka 20 juu ya mpango wake wa kutaka kuhamia Old Trafford msimu huu. ***(TalkSPORT)***

### JESUS APELEKWA SPURS
MSHAMBULIAJI wa Manchester City, Gabriel Jesus amepewa ofa ya kuhamia Tottenham Hotspur likiwa ni pigo kwa mahasimu wao wa kaskazini mwa London Arsenal, ambao wamekuwa wakihusishwa na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25. ***(Times)***

### BASTONI HAONDOKI
INTER Milan hawatamwachia mlinzi, Alessandro Bastoni mwenye umri wa miaka 23, likiwa ni pigo kwa Manchester United na Tottenham Hotspur zilizotaka kumsajili. ***(Mirror)***

### SANGARE AITAKA EPL
KIUNGO wa kati wa PSV Eindhoven, Ibrahim Sangare amejipanga kuhamia Ligi Kuu ya England, huku Liverpool, Chelsea, Manchester United na Newcastle zikimfuatilia kwa karibu mchezaji huyo wa kimataifa wa Ivory Coast mwenye umri wa miaka 24. ***(Sky Sports)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# LIVERPOOL YAIKATAA OFA YA BAYERN KWA MANE

Watoa pauni mil. 30 wenyewe wataka pauni mil. 42.8 ili kumwachia nyota huyo wa Senegal na...

**LIVERPOOL, England**

LIVERPOOL imekataa ofa ya pauni milioni 30 kutoka Bayern Munich ili kumuuza mshambuliaji wake raia wa Senegal, Sadio Mane.

Wekundu hao wameikataa ofa hiyo ya pili kutoka klabu hiyo ya Ujerumani baada ya ile ya kwanza ya pauni milioni 25 nayo kukataliwa.

Liverpool wanadaiwa kutaka takriban pauni milioni 42.8 ili kumwachia Mane mwenye umri wa miaka 30 kwa kuzingatia hesabu sawa ya Bayern ya Robert Lewandowski mwenye umri wa miaka 33.

Mane na Lewandowski wote wamebakiza mwaka mmoja kwenye mikataba yao ya sasa.

Mchezaji wa kimataifa wa Poland, Lewandowski anataka kuhamia Barcelona msimu huu wa joto baada ya muongo mmoja kule Bayern.

Mane alisema wikiendi iliyopita kwamba, angeongozwa na maoni ya umma wa watu wa Senegal kuhusu kuamua hatima yake, ambapo wengi wao wanataka aondoke hapo Anfield.

Lakini fowadi huyo hapo awali alidokeza kwamba atabakia Liverpool, akiahidi jibu "maalum" juu ya mustakabali wake kulitoa hivi karibuni. Mane ameifungia Liverpool mabao 120 tangu alipowasili kutoka Southampton kwa ada ya pauni milioni 36, Juni 2016, na kuisaidia klabu hiyo kutwaa taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka 2019 na Ligi Kuu ya England mwaka 2020.

Alitia saini mkataba mpya mwaka 2018, ambao unaisha mwishoni mwa msimu ujao.

Liverpool pia wanakabiliwa na kitendawili kuhusu mustakabali wa nyota wa Misri, Mohamed Salah, ambaye atakuwa mchezaji huru msimu wa joto wa 2023.

Salah amesema ana nia ya kubaki Liverpool msimu ujao, lakini Barcelona wanadaiwa kutaka kumsajili kama mchezaji huru mwishoni mwa msimu ujao.

Jumatano, Liverpool walihusishwa na kutaka kumnunua mshambuliaji wa Uruguay na Benfica, Darwin Nunez, mwenye umri wa miaka 22.


BREAKING NEWS
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,004,0

MECHI KALI
AUSTRIA
VERSUS
FRANCE
1 | 4.25
X | 3.54
2 | 1.81

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money ZANTEL EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# LACAZETTE ASAJILIWA RASMI LYON



**LYON, Ufaransa**

MSHAMBULIAJI wa Arsenal, Alexandre Lacazette amesajiliwa tena Lyon kwa uhamisho huru ikiwa ni miaka mitano baada ya kuondoka hapo.

Lacazette alisajiliwa Arsenal kwa pauni milioni 46.5 na amerejea katika klabu hiyo ya Ufaransa kwa mkataba wa miaka mitatu hadi Juni 2025.

Fowadi huyo wa Ufaransa alifunga mabao 54 katika mechi 158 za Ligi Kuu akiwa na Arsenal na kuwasaidia kubeba kombe la FA mwaka 2020.

Akizungumza na Canal Plus Aprili, Lacazette alisema "hajawahi kukata mawasiliano" na klabu ya nyumbani kwao ya Lyon.

Lyon walisema "tunajivunia sana na tuna furaha sana" kutangaza kurejea kwa Lacazette katika klabu aliyojiunga nayo akiwa na umri wa miaka 12, na kuongeza kuwa mkataba "umekuwa kipaumbele cha klabu kwa miezi kadhaa".

Lacazette mwenye umri wa miaka 31, alipanda kutoka timu za vijana pale Lyon na kufunga mabao 129 katika mechi 275 katika mashindano yote baada ya kuingia kwenye kikosi cha kwanza msimu wa 2009-10 na alisajiliwa na Kocha Arsene Wenger mwaka wa 2017.

Huku mkataba wa Lacazette ukikamilika mwishoni mwa Juni, kocha wa Arsenal, Mikel Arteta alikiri Aprili kwamba, Arsenal ilichukua hatari kwa kuchelewesha mazungumzo na mchezaji huyo kuhusu mkataba mpya.

"Ni makubaliano ambayo tulifanya naye. Huo ndio ulikuwa msimamo wetu na msimamo wetu unabaki vile vile - ndivyo tutakavyofanya," Arteta alisema.

"Hatari ya hilo kutokea, ilikuwapo kila mara tangu tulipofanya uamuzi huo, basi ni juu yake."

Lacazette alikuwa nahodha wa Arsenal baada ya Pierre-Emerick Aubameyang, ambaye amejiunga na Barcelona, kuvuliwa kitambaa na Arteta Desemba kwa utovu wa nidhamu.

Arsenal haijashiriki Ligi ya Mabingwa Ulaya tangu msimu 2016-17 na itacheza hatua ya makundi ya Ligi ya Europa msimu wa 2022-23 baada ya kumaliza nafasi ya tano kwenye Ligi Kuu England.

# Wakala wa Bale acheka tetesi za usajili



**MADRID, Hispania**

WAKALA wa Gareth Bale amechekeshwa na uvumi kwamba, mteja wake anaweza kujiunga na klabu ya Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, Getafe msimu huu.

Jumatano, mkurugenzi wa michezo wa Getafe, Angel Torres alitoa taarifa kwamba, wawakilishi wa Bale walikuwa wameipa klabu hiyo nafasi ya kumsajili mchezaji huyo wa Wales.

"Nilizungumza na mwakilishi wa Gareth Bale. Wamemtoa kwetu," alisema.

Mwandishi wa masuala ya usajili wa wachezaji, Fabrizio Romano, amedai kuwa Joshua Barnett - ambaye anamwakilisha Bale - amecheka mno kuhusu habari hiyo, akidai hana hata namba ya Torres.

Ingawa Getafe wanaonekana kuwa nje ya mbio, Bale bado anaweza kupata uhamisho wa kushangaza msimu huu wa joto.

Kwa mujibu wa 90min klabu ya Cardiff City imebakia kwenye kinyang'anyiro cha kuwania kuwasajili Bale na Aaron Ramsey.

HABARI MICHEZO

055,092/-

# KUNDEMBA FC YAPANDA LIGI KUU ZANZIBAR

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

TIMU ya Kundemba FC imepanda kucheza Ligi Kuu ya Zanzibar msimu ujao wa 2022/2023 baada ya kuifunga Ngome bao 1-0 katika mchezo wa ligi daraja la kwanza Kanda ya Unguja uliochezwa uwanja wa Amaan, juzi.

Kundemba imepanda daraja ikiwa imebakiwa na michezo miwili ya kumaliza ligi hiyo na imefikisha alama 59.

Ligi hiyo inaendelea ikiwa bado inatafutwa timu moja itakayoungana na Kundemba kati ya Dulla Boys yenye alama 54 na Chuoni yenye alama 52 na zote zimebakiwa na michezo miwili.

Kwa upande wa timu ambazo tayari zimeshajihakikishia kushuka daraja ni Mchangani FC yenye alama 16, Bridger Star yenye alama 18, wakati African Coast ina alama 25 na New Power ina alama 30.

Akizungumza na gazeti hili Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Ligi Kuu Zanzibar, Hashim Salum Hashim, alisema wataendelea kuwa macho kwa kuitazama kwa karibu michezo iliyobakia ya ligi hiyo.

Alisema Bodi ya Ligi haitavumilia vitendo vyovyote vya upangaji wa matokeo au viashiria vya kufanya hivyo katika muda huu ambapo ligi daraja la kwanza Kanda ya Unguja ikielekea ukingoni.

Jumla ya timu nne katika msimu huu kutokea ligi daraja la kwanza zitapanda daraja ambapo timu tatu tayari zimeshapanda ambazo ni Chipukizi na Jamhuri kutoka Kanda ya Pemba, wakati Kanda ya Unguja timu ya Kundemba FC, huku ikisubiriwa timu moja.



Vijana wakicheza mpira wa makaratasi katika viwanja vya Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Luiza Mbutu ajipanga kuunganisha wanamuziki

**Na Sabato Kasika**

MWENYEKITI wa Chama cha Muziki wa Dansi Tanzania (CHAMUDATA), Luiza Mbutu, amesema katika kipindi chake cha uongozi cha miaka mitatu, atahakikisha anaunganisha wanamuziki wote Tanzania na kuwa kitu kimoja.

Aidha, amesema atajitahidi chama kuwa na ofisi na pia kila mwanamuziki kuwa na kadi ya chama hicho, na kwamba bila mwanamuziki kuwa nayo hatatambuliwa na Baraza la Sanaa Tanzania (BASATA).

"Hiyo ni baadhi ya mkakati yangu ambayo nitaitekeleza kwa muda ambao nitakuwa kwenye uongozi nikishirikiana na viongozi wenzangu, kwani hakuna umoja miongoni mwa wanamuziki nchini," amesema Luiza.

Amesema CHAMUDATA ni kiunganishi kikubwa cha wanamuziki wote nchini, na kwamba bahati mbaya hawakuunganishwa na kusababisha kutokuwapo umoja miongoni mwao.

"Mimi nitajitahidi kwa kushirikiana na wenzangu kuhakikisha malengo tuliojiwekea yanatimia kwa ajili ya manufaa ya wanamuziki wote na kuhakikisha chama kinaendelea kuwa hai," amesema.

Ameongeza kuwa, kwa sasa wanandelea kupanga kamati mbalimbali, kwa ajili ya kufanikisha kile ambacho wamekusudia kukifanya kwa manufaa ya chama na wanamuziki kwa ujumla.

Luiza amesema, chama hicho kilipoteza hadhi na kusababisha kionekane hakina umuhimu kwa wanamuziki, na kwamba yeye na viongozi wenzake hawana budi kurejesha hadhi hiyo.

"Mtuombee katika majukumu haya ili tuweze kufikia malengo ya kuinua muziki wa dansi nchini ili urudi kwenye hadhi kama zamani kwani unakabiliwa na changamoto nyingi," amesema.


SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01.11/06/22 | 19:00 | Faroe Islands vs Lithuania | 2.31 | 2.90 | 3.30 |
| 02.11/06/22 | 19:00 | Ireland vs Scotland | 2.27 | 3.05 | 3.20 |
| 03.11/06/22 | 21:30 | Arsenal Sarandi vs Banfield | 2.70 | 3.05 | 2.65 |
| 04.11/06/22 | 21:45 | Montenegro vs Bosnia and Herzegovina | 2.65 | 3.00 | 2.70 |
| 05.11/06/22 | 22:00 | Charlotte FC vs New York Red Bulls | 3.05 | 3.35 | 2.20 |
| 06.11/06/22 | 22:00 | Girona vs Tenerife | 2.32 | 3.10 | 3.05 |
| 07.12/06/22 | 00:00 | Sarmiento vs Argentinos Juniors | 3.05 | 3.15 | 2.28 |
| 08.12/06/22 | 01:00 | Cuiaba MT vs Bragantino SP | 2.80 | 3.05 | 2.55 |
| 09.13/06/22 | 01:00 | Tombense MG vs CSA AL | 2.70 | 2.75 | 2.90 |
| 10.12/06/22 | 03:00 | Internacional vs Flamengo | 2.80 | 3.30 | 2.37 |
| 11.12/06/22 | 07:00 | Renofa Yamaguchi vs Fagiano Okayama | 3.05 | 2.95 | 2.44 |
| 12.12/06/22 | 08:00 | Mito Hollyhock vs Montedio Yamagata | 2.60 | 3.10 | 2.65 |
| 13.12/06/22 | 08:00 | Blaublitz Akita vs Omiya Ardija | 2.41 | 3.00 | 3.05 |
| 14.12/06/22 | 19:00 | Colon Santa Fe vs Union Santa Fe | 2.43 | 2.95 | 3.05 |
| 15.12/06/22 | 21:30 | Godoy Cruz vs Racing Club | 2.47 | 3.25 | 2.75 |
| 16.12/06/22 | 22:00 | Vasco da Gama vs Cruzeiro | 2.65 | 2.90 | 2.80 |
| 17.12/06/22 | 22:00 | Sporting Kansas City vs New England Revolution | 2.85 | 3.40 | 2.28 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE
"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

IJUMAA - 10/06/2022

| MUDAVV | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 2194 | South Korea vs Paraguay | 1.85 | 3.36 | 4.48 |
| 15:00 | 1916 | Estudiantes de LP Reserve vs CA Aldosivi Reserve | 1.82 | 3.48 | 3.78 |
| 15:00 | 3285 | Panama Youth vs Comoros Youth | 1.93 | 3.14 | 3.78 |
| 16:00 | 3529 | Zvezda 2005 Perm W vs FK Rostov W | 2.11 | 3.14 | 3.24 |
| 16:30 | 3190 | CSKA Moscow W vs Chertanovo Moskva W | 1.17 | 5.31 | 17.69 |
| 17:00 | 1974 | Defensa Y Justicia Reserve vs CA Lanus | 2.80 | 3.24 | 2.30 |
| 17:00 | 2241 | Rosario Central Reserve vs Huracan Reserve | 2.15 | 3.33 | 2.99 |
| 17:00 | 5106 | Patronato Reserve vs Gimnasia de la Plata Reserve | 2.99 | 3.33 | 2.15 |
| 18:00 | 1353 | Finland U21 vs Norway U21 | 2.65 | 3.49 | 2.29 |
| 18:00 | 2313 | MKS Kluczbork vs Warta Gorzow Wielkopolski | 2.26 | 3.33 | 2.79 |
| 18:00 | 2633 | FK Silas vs FA Siauliai B | 2.18 | 3.63 | 2.74 |
| 18:00 | 2727 | TS Sokol Aleksandrow Lodzki vs Mamry Gizycko | 2.06 | 3.49 | 3.05 |
| 18:00 | 4009 | Unia Skierniewice vs Mlks Wissa Szczuczyn | 1.46 | 4.31 | 5.48 |
| 18:30 | 1608 | Rekord Bielsko Biala vs Karkonosze Jelenia Gora | 1.37 | 4.71 | 6.28 |
| 18:30 | 1639 | MP Mikkeli vs TPS Turku | 3.72 | 3.43 | 1.85 |
| 18:30 | 2289 | Pif Jalkapallo vs EIF Ekenas | 3.78 | 3.68 | 1.78 |
| 18:30 | 4363 | CA Rentistas vs Deportivo Maldonado | 2.60 | 3.18 | 2.50 |
| 18:30 | 5089 | MFK Zarnovica vs MSK Fomat Martin | 5.91 | 4.53 | 1.41 |
| 18:30 | 5783 | Lechia Tomaszow Mazowiecki vs Legia II Warszawa | 2.16 | 3.57 | 2.79 |
| 18:45 | 1577 | Ol. Medea vs HB Chelghoum Laid | 2.06 | 3.05 | 3.49 |
| 18:45 | 2992 | MC Magra vs RC Relizane | 1.25 | 5.13 | 9.28 |
| 18:45 | 3395 | MC Alger vs MC Oran | 1.78 | 3.15 | 4.53 |
| 18:45 | 4081 | NA Hussein Dey vs US Biskra | 2.90 | 2.95 | 2.41 |
| 19:00 | 1049 | Taarnby FF vs Skovshoved | 1.47 | 4.32 | 5.30 |
| 19:00 | 1074 | FC Neptunas Klaipeda vs FK Minija | 1.37 | 4.81 | 6.09 |
| 19:00 | 1230 | PK-35 Vantaa W vs Nurmijarven Jalkapalloseura | 1.01 | 12.72 | 34.25 |
| 19:00 | 1945 | FC Lokomotiv Moscow W vs Ryazan Vdv W | 1.20 | 4.92 | 15.74 |
| 19:00 | 2469 | Pepo Lappeenranta vs Japs | 2.19 | 3.43 | 2.84 |
| 19:00 | 3394 | Denmark U21 vs Scotland U21 | 1.40 | 4.22 | 6.67 |
| 19:00 | 3599 | Zaglebie II Lubin vs Stal Brzeg | 1.66 | 3.87 | 4.21 |
| 19:00 | 4635 | Azerbaijan vs Slovakia | 4.53 | 3.32 | 1.82 |
| 19:00 | 5342 | Moldova vs Latvia | 2.68 | 3.03 | 2.73 |
| 19:00 | 5814 | Riteriai B vs FK Vilnus Bfa | 1.72 | 3.93 | 3.78 |
| 19:30 | 5047 | FC Sydvest 05 vs B 1909 Odense | 2.69 | 3.77 | 2.16 |
| 19:45 | 4598 | TUS Bad Gleichenberg vs Union Gurten | 2.86 | 3.79 | 2.06 |
| 19:45 | 5789 | SC Weiz vs FC Wels | 1.93 | 3.87 | 3.09 |
| 20:00 | 2314 | Tolo IF vs Vastra Frolunda IF | 5.11 | 4.52 | 1.46 |
| 20:00 | 2934 | Turkey U21 vs Kazakhstan U21 | 1.26 | 5.10 | 8.82 |
| 20:00 | 3929 | Angered BK vs Stenungsunds IF | 2.95 | 3.44 | 2.12 |
| 20:15 | 1514 | Ahlafors IF vs Lidkopings FK | 1.77 | 3.59 | 3.89 |
| 21:00 | 1364 | Kosovo U21 vs England U21 | 14.82 | 6.92 | 1.13 |
| 21:00 | 2804 | River Plate (URU) vs CS Cerrito | 1.74 | 3.53 | 4.11 |
| 21:45 | 1291 | Austria vs France | 4.25 | 3.54 | 1.81 |
| 21:45 | 1460 | Albania vs Israel | 2.27 | 3.23 | 3.13 |
| 21:45 | 1675 | Athlone Town vs Cobh Ramblers | 2.85 | 3.34 | 2.23 |
| 21:45 | 1687 | Wexford Youths vs Treaty United | 2.13 | 3.24 | 3.10 |
| 21:45 | 4169 | Andorra vs Liechtenstein | 1.84 | 3.33 | 4.44 |
| 21:45 | 4261 | Belarus vs Kazakhstan | 2.37 | 2.97 | 3.22 |
| 21:45 | 4910 | Longford Town vs Bray Wanderers | 1.89 | 3.43 | 3.58 |
| 21:45 | 4992 | Denmark vs Croatia | 1.90 | 3.49 | 3.89 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Ijumaa Juni 10, 2022
Nipashe



## Liverpool yaikataa ofa ya Bayern kwa Mane



Ofisa Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Ligi Tanzania Bara, Almasi Kasongo (katikati) akiwa na kombe jipya ambalo atakabidhiwa mshindi wa Ligi Kuu Tanzania Bara. **PICHA: TFF**

# BINGWA LIGI KUU BARA KUSOMBA SH. MIL. 600

## ●●●Sh. milioni 500 ni bonasi, huku Sh. milioni 100 ndio zawadi ya bingwa na wanaoshuka daraja kupewa...

**Na Adam Fungamwango**

BODI ya Ligi Tanzania Bara jana imesema kuwa jumla ya Sh. bilioni 1, milioni 800 na Elfu 20 zitatolewa kama zawadi kwa timu zote 16 zinazoshiriki ligi, huku bingwa akitarajiwa kusomba kiasi cha Sh milioni 600.

Akizungumza jana kwenye mkutano wa bodi hiyo na Waandishi wa Habari, Ofisa Mtendaji Mkuu, Almasi Kasongo amesema zawadi hizo zimegawanyika sehemu mbili, ya kwanza ikiwa ni bonasi na zingine ikiwa ni zawadi za timu tatu zilizoshika nafasi za juu kwa mujibu wa kanuni.

Amesema bonasi zimetolewa na wenye haki ya kushusha matangazo, huku zawadi za bingwa hadi nafasi ya tatu zikitolewa na wadhamini wa Ligi Kuu.

Pia bodi hiyo imetambulisha kombe jipya ambalo litakabidhiwa kwa timu bingwa msimu huu na misimu mingine inayofuata.

"Pesa zilizotumika kwa zawadi za washindi na bonasi ni shilingi bilioni moja, milioni mia nane, na elfu 20 ambazo timu zote 16 zitapata na kwa utafiti wetu ni kwamba Tanzania inakuwa ni ya pili kwenye Ukanda wa Chini ya Sahara kwa ligi yetu kukuwa na zawadi kubwa kwa washindi, ukiondoka ligi za Afrika Kaskazini. Nchi ya kwanza kwenye ukanda huu ni Afrika Kusini na sisi tuko kwenye nafasi ya pili," alisema Kasongo.

Katika mchanganuo huo, alisema kuwa timu nne za juu zinapata bonasi pamoja na pesa zao za ushindi kutoka kwa wadhamini, kuanzia ya nne mpaka ya 14 zitapata bonasi, huku ya 15 na 16 ambazo zitashuka zenyewe zitapata kiinua mgongo, pesa ambazo zitatolewa na Bodi ya ligi kama 'mkono wa kwa heri' au mchango kwa ajili ya maandalizi ya kwenda kucheza ligi ya Championship.

Kwa mujibu wa Bodi ya Ligi, Bingwa msimu huu atapata jumla ya Sh. Milioni 600, kiasi cha Sh. Milioni 500 ikiwa ni bonasi na zawadi ya ubingwa ikiwa ni Sh milioni 100.

Mshindi wa pili imetajwa kuwa anaondoka na jumla ya Sh. milioni 300, kiasi cha Sh milioni 250 ni bonasi na zawadi wa mshindi wa pili ikiwa ni Sh. milioni 50, wakati mshindi wa tatu yeye ataondoka na Sh. milioni 255, bonasi ni Sh. milioni 225, na Sh milioni 30 ikiwa ni zawadi ya mshindi wa tatu wa Ligi Kuu.

Bodi ya Ligi ilisema mshindi wa nne bonasi yake ni Sh. milioni 200, wa tano atapata kiasi cha Sh. milioni 65, wa sita Sh milioni 60, nafasi ya saba atalamba Sh. milioni 55, huku timu itakayoshika nafasi ya nane, itaondoka na kitita cha Sh milioni 50, wa tisa Sh. milioni 45 na wa 10, atapata Sh. milioni 40.

Timu itakayoshika nafasi ya 11 bonasi yake ni Sh. milioni 35, na wa 12. Sh. milioni 30 na timu ya 13 itapata Sh. milioni 25.

Timu ya 14 ambayo itacheza mechi ya mchujo itapata Sh milioni 20 na timu ya 15 na 16 ambazo zitashuka daraja, zenyewe zitapewa Sh milioni 10 kila moja.

## Poulsen: Stars ilizidiwa ubora na Algeria

**Saada Akida na Shufaa Lyimo**

BAADA ya kukubali kichapo cha mabao 2-0 kutoka kwa Algeria, Kocha Mkuu wa timu ya Taifa ya Tanzania, (Taifa Stars), Kim Poulsen amesema wachezaji wake walikuwa na wakati mgumu wa kupambana na nyota bora na imara.

Stars juzi ilifungwa mabao 2-0 katika uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam katika mechi ya pili ya kufuzu kushiriki fainali za mataifa ya Afrika, AFCON, zinazotarajiwa kufanyika mwaka 2023 nchini Ivory Coast.

Akizungumza na gazeti hili mara baada ya mchezo huo, Poulsen alisema hawakufikia malengo ya kupata ushindi kwa sababu ya timu pinzani kuwa na wachezaji wenye ubora wa hali ya juu.

Alisema licha ya ubora wa wapinzani wao, lakini anawapongeza wachezaji wake kwa kupambana na kuonesha mchezo mzuri mbele ya timu bora kama Algeria.

"Wachezaji wanatakiwa kupongezwa kwa sababu ni ngumu kucheza na Algeria na ukatawala mpira na kufanya mashambuliza kadhaa, kwa kiwango kilichooneshwa na wachezaji wangu nina imani timu yetu ina mabadiliko makubwa na tutafanya vizuri huko mbeleni," alisema.

"Tulikuwa na makosa madogo madogo ambayo yalituadhibu, tumeumia hatujapata matokeo na mchezo huu umetupa somo na Septemba itatupa mwanga wa wapi tutakuwa michuano hii ya kufuzu AFCON," alisema Poulsen.

Alisema kutokana na wachezaji kupambana na hatimaye kupoteza wanaenda kujiuliza wamepoteza vipi na kujiandaa na michuano ya CHAN ambayo kwa sasa iko mbele yao kwa kuanza na Sudan.

Poulsen alisema michuano ya CHAN dhidi ya Sudan watacheza vizuri, lakini pia watatafuta matokeo mazuri na kuibuka na ushindi ili kusonga mbele zaidi.

"Michuano ya CHAN lakini pia anahitaji mechi nne za kirafiki za kimataifa ili kujiandaa na mchezo dhidi ya Uganda ambao ni mechi ya tatu ya hatua ya makundi ya AFCON," alisema kocha huyo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >